

YAKINI

 Asante, Ndugu Shakarian. Hebu tuendeleo tu kusimama kwa dakika chache. Nina hakika, katika kusanyiko la ukubwa huu, kuna haja nyingi, watu walio wagonjwa, wahitaji, na kwa hiyo hebu tuinamishe tu vichwa vyetu kwa dakika moja kwa maombi. Hapa kuna haja nyingi zimewekwa hapa, pia, na lesu.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja sasa katika Jina la Bwana Yesu, tukijua hili, ya kwamba Wewe uliahidi ya kwamba ungesikia na kuyajibu maombi yetu. Nami nakuomba uturehemu, utusamehe dhambi zetu. Nasi tunafundishwa, katika Maandiko, ya kwamba, “Unatusamehe dhambi zetu zote, na kuyaponya magonjwa yetu yote.” Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba hili litafanywa alasiri ya leo sasa, kwa sababu tunaomba katika Jina la Bwana Yesu.

³ Juu ya lesu hizi na haja, tumefundishwa katika Maandiko, jinsi ambavyo, “Kutoka kwenye mwili wa Paulo zilichukuliwa lesu na nguo, nao pepo wachafu wakawatoka watu, nao wakapona.” Sasa, Wewe ni Yesu yeye yule leo. Nasi tunasimama, kwa wingi, tukiomba ya kwamba utayajalia mambo haya.

⁴ Kunazo, hapana shaka, haja nyingi jengoni leo, za watu wengi sana walio na haja katika saa hii. Yakidhi mahitaji yao, Bwana, ya kimwili na ya kiroho pia, kwa kuwa tunaomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

Vema. Asante, ndugu.

⁵ Tulizoea kuimba wimbo mdogo, miaka kadhaa iliyopita, “Mazungumzo Madogo Pamoja Na Yesu Hulifanya Sawa.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁶ Sasa, ninaamini Ndugu Williams ndio kwanza amalize kusema kuna kiamshakinywa asubuhi. Na sasa, siamini nimepata kusikia ambako mwaka ujao utakuwa. [Ndugu mmoja anasema, “Papa hapa.”—Mh.] Papa—papa hapa tena. Papa—papa hapa tena. Vema, mahali pale pale. Mahali pale pale, hilo ni zuri sana. Naam. Hilo ni ninii sana . . .

⁷ Watu wanapaswa kuabudia Yerusalemu, hiyo ni Tucson, sio—sio hapa chini. Mnaona? Sasa, ninyi mko huko chini ya kilima. Yeriko iko chini ya kilima, kutoka Yerusalemu, mwajua. Kwa hiyo, hiyo ni Yerusalemu kule chini. Mnaona? [Ndugu fulani basi anasema, “Tunatarajia mwujiza mkubwa kule.”—Mh.] Mlisikia hilo?

⁸ Kwa hiyo “Watu wanapaswa kumwabudu Mungu, kila mahali,” Yesu alisema, mwajua. “Si Yerusalemu, wala hapa au kwenye mlima huu, bali wamwabudu katika Roho na katika

Kweli.” Hilo ndilo jambo muhimu, “Katika Roho na katika Kweli.”

⁹ Sasa, mimi, kwa kawaida, ninapozungumza, mimi ni mwenda pole sana. Ni—nilikuwa nikipendewa na Ndugu Velmer Gardner, hivi majuzi usiku, angeweza kuja hapa na kusema mengi katika dakika kumi na tano kuliko ninavyoweza kuweka katika saa tatu. Jamani!

¹⁰ Si—sijui kama nilipata kuwaambia hili ama la. Nilipokuwa m—mtoto mdogo, mimi... baba yangu alikuwa mpanda farasi, mwajua. Naye alikuwa akiwapanda farasi na kuwafunza, akafuatana na maonyesho ya wachunga ng’ombe, akirusha risasi, risasi za kuwashtua. Naye... Niliwazia, mwajua, nilipofikia umri wa kama miaka kumi na miwili, ninapaswa kufuata nyayo za baba yangu. Kwa hiyo wakati wangelima na maskini yule farasi mzee, huko Indiana, mwajua, mpaka akachoka sana karibu asingeweza kusogea. Ni—ningempata baba yangu, wakati alipozunguka na plau, mwajua, huko mbali nyuma ya shamba. Nami ningeshuka kule ambako walikuwa na kihori cha kunyweshea kilichotengenezwa kwa gogo.

¹¹ Ni wangapi waliopata kuona moja ya hivyo vihori vya kunyweshea? Jamani, angalieni Wakentaki walio hapa ndani!

¹² Kwa hiyo, loo, nilikuwa na wakati mzuri, ninashuka na kutia manyoya ya farasi majini, mwajua, nikaangalia yakigeuka, kile tulichokiita, “nyoka wa manyoya ya farasi.” Ni hayo ninii... Mnajua, ukiyagusa, basi yangesogea. Nao nyuki...

¹³ Ningewaleta ndugu zangu wadogo na wote, na kuwaweka kule chini. Ndipo ningemchukua maskini yule farasi wa kulima, mwajua, na kunyakua lijamu na hatamu kutoka kwake upesi sana, na kuchukua matandiko ya baba, konzi ya vichomanguo na kuviweka chini ya tandiko, na kuvuta chini mkanda wake. Ninge—ningeruka huko juu. Maskini farasi, mzee na amechoka, wala asingeweza kuinyanyua miguu yake kutoka ardhini. Angepiga tu makelele, mwajua. Nami ningeitupa hiyo kofia huku. Jamani! Nilidhani nilikuwa mpanda farasi.

¹⁴ Basi nikawazia nyote mlinihitaji huku nje, Arizona, kuwafunza farasi wenu, mwajua. Kwa hiyo, yapata umri wa miaka kumi na saba, kumi na minane, nikatoroka, nikaja huku ambako walikuwa na ma—mashindano ya wafuga ng’ombe. Vema, nikawazia, “Jamani, laiti ningeweza tu kuingia kwenye yale mashindano ya wafuga ng’ombe, nitawaendeshea farasi. Nitajipatia pesa.”

¹⁵ Kwa hiyo, ninakumbuka, mpanda farasi wa kwanza alitokea. Alikuwa akimpanda yule aliyeitwa... Ninaamini wanamwita, “Haramia wa Kansas.” Yeye ni farasi mkubwa mno, jamaa mkubwa mweusi yapata urefu wa mikono kumi na saba. Yeye ni farasi mzito kweli, mwenye nguvu. Nikawaza, “Vema, kama

jamaa huyo anaweza kumpanda, nami pia ninaweza.” Basi mpandaji huyu maarufu akaenda pale.

¹⁶ Nami nilikuwa nimeketi karibu na lile boma, mwajua, pamoja na zizi walimokuwamo wachunga ng’ombe hawa wote walioharibika sura, mwajua. Sikuwa nimeharibu sura yangu kabisa kama wao walivyokuwa, bali nilidhani mimi ni mpandaji bora vivyo hivyo. Kwa hiyo wao... Nilikuwa nimemwendesha maskini huyo farasi wa kulima, basi kwa nini nisimwendeshe huyo?

¹⁷ Kwa hiyo aliposhuka kutoka kwenye banda lake, jamani, farasi huyo angeweza kuweka miguu yote minne katika sufuria ya kuoshea. Akarukaruka na kuzungukazunguka pale, mara chache. Ndipo matandiko yakarushwa upande mmoja, na mpanda farasi upande mwingine. Basi gari dogo la mizigo likamchukua farasi, nalo gari la kuchukulia wagonjwa likambeba mpandaji. Nikajua huyo hakuwa yule farasi mzee wa kulima niliyezoea kumpanda.

¹⁸ Mtangazaji akashuka, akasema, “Nitampa mtu yeyote,” kasema, “dola hamsini.” Hizo zilikuwa ni hela nyingi wakati huo. “Dola hamsini, ambaye anaweza kumwendesha, sekunde *kadhaa* akiwa juu yake.” Naye... Ni—nilikuwa tu nikitetemeka. Akanijia akasema, “Wewe ni mpandaji?”

Nikasema, “La, bwana.”

¹⁹ Wakati nilipookolewa kwanza na kuwekwa wakfu, kanisa la Baptisti la Kimishenari, nilikuwa nikibeba Biblia kote, mwajua, nami nilitaka mtu aniulize iwapo nilikuwa mhubiri, mwajua. Lakini kila wakati, mtu fulani akisema, “Wewe ni mhubiri?”

Ningesema, “Hakika.”

²⁰ Siku moja nilikuwa huko St. Louis. Nilikuwa ndio kwanza nikutane na ndugu yetu wa Kibaptisti, nami nilikuwa huko St. Louis. Ndipo nikamsikia jamaa jina lake Robert Daugherty. Wengi wenu huenda mkamjua. Naye alikuwa katika mkutano wa hema. Alikuwa ni ndugu wa Kipentekoste. Jamani! Mtu huyo alihubiri hata akawa samawati usoni. Naye a—a—alihubiri mpaka akazama chini. Ungeweza kumsikia akizua pumzi yake, umbali wa majengo mawili ya mji, pasipo na kipaza sauti, pia. Na kuzuia tu pumzi yake, kisha anarudi tena, akihubiri.

Tangu wakati huo, mtu akisema, “Wewe ni mhubiri?”

²¹ Nilisema, “La. Ni—ninawaomba tu wagonjwa.”

²² Njia zangu za kale pole, za Kibaptisti, haziziwazii upesi hivyo, kwa hiyo nivumilieni tu, mwajua. Nanyi mwajua ni Maandiko, yaliyosema “kuvumiliana nao walio dhaifu,” kwa hiyo huyo ni mimi. Kwa hiyo ninashukuru ya kwamba nyote mmejaribu kufanya hivyo juma hili, na mmeifanya kazi nzuri sana. Saa nne usiku, wakati nilipopaswa kuwa nyumbani na kitandani, huku nikiwaweka ninyi nje.

²³ Lakini, kwa kweli, alasiri ya leo, nitajaribu kuharakisha na kutoka moja kwa moja. Ningali nina kuendesha gari kwingi ninakotakiwa kufanya alasiri ya leo, kusudi nirudi hapa asubuhi.

²⁴ Na, kwa hiyo, ni—ninawathamini, hata hivyo. Na endapo sitapata nafasi ya kusema jambo hili kwenye wakati mwingine wowote, nawashukuru, sana, kila mmoja, ninyi wahudumu wote, nanyi wafanyabiashara Wakristo. Hivi, ni furaha kweli, kwenu kunialika, na kuniruhusu nje hapa na kutia plagi yangu ndogo pamoja nanyi ndugu. Ndugu Shakarian, Ndugu Williams, na wa—wanaume wote. Hakika ninashukuru.

²⁵ Na kwa nini hukusema “amina” muda mfupi uliopita, Tony, wakati nilipozungumza kuhusu Tucson? Hata sikumsikia. Huyu ndiye mwindaji hodari kuliko wote Arizona wakati nikiwa Indiana, mnaona, ila hiyo ni baada ya mimi kwenda Indiana. Mliona picha yake gazetini hivi majuzi? Ambapo... Inatubidi kubadilisha hilo, Tony.

²⁶ Kwa hiyo sasa, kumbukeni, kesho usiku, ile dhifa kwenye... pamoja na Ndugu Oral Roberts.

²⁷ Na, sasa, kabla hatujalikaribia Neno. Ni—nilikuwa nizungumze alasiri ya leo juu ya *Kuhesabu Kinyumenyume*. Nami nikafikiri ya kwamba—ya kwamba ningalikuja hapa, mngekuwa mngali mmekeki hapa kwenye saa moja. Loo, loo, kuhusu yale sayansi imeweza kufanya, na halafu yale Mungu ameweza kufanya, mnaona. Na kwa hiyo tunaishi katika wakati tofauti na tuliokuwa tukiishi, kimwili na kiroho pia. Kwa hiyo tuna—tunashukuru kwa ajili ya mafanikio yetu katika milki za kiroho, kama vile sayansi ilivyo katika—katika milki zao za kawaida, milki za kisayansi. Sasa hebu, kama hamjali, tena...

²⁸ Mwajua, huenda ukaimba kupita kiasi. Sioni hasa jinsi ungeweza, kama ukiimba kama kwaya ya Ndugu Outlaw, muda mfupi uliopita, wakati nilipokuwa nimesimama pale nikiisikiliza, hao wakienda, “Juu, juu, juu, juu.” Na, lakini, na tena, huenda ukala kupita kiasi. Huenda ukanywa kupita kiasi. Huenda ukafanya kazi kupita kiasi. Lakini sidhani unaweza kuomba kupita kiasi. Biblia ilisema, “Nataka wanaume wasali kila mahali, wakiinua mikono mitakatifu.” Mnaona?

Kwa hiyo hebu tuinamishe vichwa vyetu tena, kwa dakika moja tu.

²⁹ Baba wa Mbinguni, tu—tunapenda kuzungumza na Wewe. Nami ninawazia juu ya wanaume, jinsi ninavyopenda, kujua ya kwamba wako mjini, kuwapa tu mkono na kuzungumza nao. Sote tuna hisia hizo. Na ni kuu zaidi sana vipi kwa majaliwa ya kuzungumza na Wewe, Bwana wetu na Mwokozi wetu! Basi mioyo yetu inadundadunda, kuwa mbele za mmoja kwa mwingine, na basi ni zaidi sana vipi wakati tunapojua tuko katika Uwepo Wako wa Kiungu!

³⁰ Nasi tunajua Wewe upo hapa, kwa sababu Wewe ulisema, “Popote.” Kama ni ulimwenguni kote, ama kote ulimwenguni, ama popote pale, “Popote wawili ama watatu wanapokusanyika katika Jina Langu nitakuwa pale miongoni mwao.” Nasi tunajua ya kwamba Maandiko hayo hayawezi kushindwa. Ahadi hiyo ni ya Kiungu. Ilitoka katika midomo ya Mwokozi. Na kwa hiyo, labda sisi ni... dhamiri yetu na ninii yetu... Dhambi ya kutokuamini kwetu imetutenganisha, mbali sana, hata huenda tusiweze kutambua Wewe upo hapa. Lakini Wewe upo hapa vile vile tu, kwa kuwa Wewe hutimiza ahadi Yako.

³¹ Na sasa, Wewe ulisema, “Kama wataomba lolote, kuhusu jambo moja, basi watapewa.” Na, Baba, ja—jambo lililo kuu sana ambalo ningeweza kuwazia, kwenye wakati huu tu na kwa ajili ya kusanyiko hili ni, tulishe, Bwana, kwa Mana ya kiroho itokayo kwa Mungu, kutoka Mbinguni. Tujalie, Bwana. Tulishe kwa Neno Lako. “Neno Lako ni Kweli.” “Na mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Basi tunapolisoma Hilo, jalia Roho Mtakatifu alipeleke kwenye kila moyo, na kuligawa miongoni mwetu leo kadiri ya haja zetu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwana Wako. Amina.

³² Sasa, mara nyingi, kadiri nilivyosema, wahudumu na watu, tunasikilizana sisi kwa sisi tunapozungumza. Kisha tunaandika mafungu ya Maandiko ambayo mhadumu mwingine ameyazungumzia, ama mtu fulani. Na—nami sikuzote ninafanya hivyo, nikishuka barabarani. Nina kipande kidogo cha karatasi, kijitabu kidogo, kilichowekwa ka... karibu nami. Ndipo Andiko litaingia niani mwangu, ninaliandika hilo chini. Basi muda si muda mwajua... Sasa, ninyi nyote mna hatia ya hilo, sivyo? Sisi hufanya hivyo. Halafu basi, baada ya kitambo kidogo, Roho Mtakatifu ataliuisha hilo kwetu. Kisha tunapata wazo lingine, ndipo inanibidi tu kuegesha gari kando ya barabara na kuandika mambo fulani.

³³ Basi—basi hiyo ndiyo njia, basi, ninapofikia wakati wangu wa kuzungumza, nitayapitia mambo hayo tena. Nitaanza kuyawazia, nikiyaendea marejeo ya Maandiko, kisha ninayaandika hayo marejeo ya Maandiko. Basi wakati nikiliendea, ninakumbuka yale Maandiko yanayosema, kisha nazungumza kutoka hapo. Karibu sote hufanya hivyo.

³⁴ Sasa nitasoma karibu tu kifungu kimoja, kutoka kwenye kitabu cha Wafilipi tena. Nilikuwa nikisoma kutoka Wafilipi hivi majuzi usiku, juu... Jumatano usiku huko pamoja na Ndugu Shores kwenye Assembly of God, nilipozungumza juu ya somo la *Kutambulishwa Pamoja Naye*. Na sasa ninataka kusoma kutoka kwenye mlango wa kwanza wa Wafilipi, kwa ajili ya alasiri ya leo, kwenye kifungu cha 20. Na sasa hebu tusikilize kwa njia ya maombi tunaposoma.

Kama vile nilivyotazamia sana, na kutumaini,

kwamba sitaaibika kamwe, bali kwa lililo uthabiti, kwa uthabiti wote, . . . siku zote na sasa vivyo hivyo Kristo ataadhimishwa katika mwili wangu; ikiwa kwa maisha yangu, au ikiwa kwa mauti yangu.

Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida.

Ila ikiwa kuishi katika mwili, kwangu mimi ni matunda ya kazi; basi nitakalolichagua silitambui.

³⁵ Nilikuwa nikiwazia jambo hili, nami nikawazia ningetumia wazo dogo linalojulikana, neno moja tu.

³⁶ Unasema, “Ndugu Branham, ‘neno moja,’ kwa huu, labda watu elfu moja wanaoketi hapa?” ‘Neno’ moja tu?” Vema, kama ni neno linalofaa. Mnaona?

³⁷ Nami ninataka kujaribu, kama Roho Mtakatifu, Yeye anayetuvuvia, kujenga ninii dogo, kupata muktadha mdogo kwenye somo langu. Ninataka kuliita: *Yakini*.

³⁸ *Yakini*. Sasa, nilikuwa nikiangalia katika kamusi, kutaka kujua. Nilipokuwa nikiliangalia neno, *kujitambulisha*, nilipata neno hili, *yakini*. Nalo *yakini*, kulingana na kamusi ya Webster, ni, inasema ni “kamilifu lenyewe; lisilo na kikomo katika nguvu zake; kimsingi ni mkataa.”

³⁹ *Yakini*. Linatumika mara nyingi. Ni “neno la mwisho” Ni “amina.” Unawasikia watu wakisema, “Yakini, ndilo hilo.” Hilo ndilo “jambo la mwisho.” Ha—halina “kikomo.” Mnaona? Hilo, hilo linachukua “tangu hapa na kuendelea.” Hakuna “kitu kingine njiani mwake.” Ndi—ndilo “lenye mamlaka ya juu kabisa.” Ni “mkataa.” Na mkataa ni, wakati, kimsingi mkataa, kwa sababu “umefika mwisho.” Ni “amina.” Hivyo tu.

⁴⁰ Sasa, chochote, na kufungamanishwa na kila ufanisi ulio mkuu, imekuwa ni yakini. Kwa kila mtu, na kila kitu ambacho kilifanywa, ama kimefanywa, hasa, kumekuwako na yakini iliyohusishwa nacho. Hapana budi pawe na kitu, kwa kuwa ndiyo nguzo ya mwisho ya kufungia. Naye mwanadamu hawezi, kwa njia yoyote, kufanikisha chochote mpaka afikie mahali ambapo wanatambua ya kwamba kuna yakini.

⁴¹ Wakati mmoja, katika ofisi ya da—daktari, nilikuwa nikizungumza na daktari. Naye akasema, “Vema, na—nakwambia, Billy.” Kasema, “Ni kweli kwamba—kwamba ninaamini ya kwamba mtu anaweza kujitwalia imani ya kutosha, hata angeweza kutoka hapa na kuugusa mti huu na kupona.”

⁴² Nikasema, “Lakini, daktari, mtu kamwe angewezaje kujitwalia imani ya kutosha kuugusa mti na kupona? Mnaona? Kwa sababu, hamna msingi kwa hilo. Hamna—hamna mahali unapoweza kuifunganishia, kwa sababu si—si—si ninii, kimaandiko, si msingi.”

43 Bali huna budi kuwa na kitu fulani unachoweza kujifungia, kujua ya kwamba Hiki ndicho. Hiyo ndiyo... Mambo mengi madogo huenda yakaelekeza kwake, lakini Hilo ndilo Neno la mwisho, jambo la mwisho. Hiyo ndiyo sababu mimi daima nimeamini katika—katika Neno.

44 Nami najua, labda ushuhuda mdogo unaokuja moyoni mwangu sasa hivi tu, huenda usiwe wa kufaa sana, lakini na—natumaini ya kwamba ha—halitachukiza. Naye mke wangu anayeketi pale, na, loo, wengi hapa, wanajua ya kwamba hilo ni kweli. Kulikuwako na...

45 Nilikuwa nikitembea na m—m—msichana mdogo aliyekuwa kwenye...kutoka kwenye kanisa la Baptisti huko Milltown, Indiana, ambalo nilikuwa mchungaji wake. Basi msichana huyo aliishakuwa mikutanoni na kuona yale Mungu aliyofanya. Na, loo, tulikuwa tu ni marafiki, marafiki wazuri tu. Na baadaye sote wawili tulikuwa... Aliolewa na kijana mwanamume mzuri. Ha—halafu basi, baadaye, mimi nikaoa. Na hatujaonana sisi kwa sisi, kwa miaka.

46 Baba yake alikuwa ni rafiki yangu msiri sana. Jina lake lilikuwa ni Lee, Marion Lee. Nami ninakumbuka, usiku mmoja, Maandiko, asingeweza—asingeweza kuyatatua. Akasema, “Ndugu Branham, si—sikutilii shaka. Lakini,” kasema, “unajua, daima nimefundishwa *hili*.” Yeye alikuwa ni—alikuwa ni Mnazarayo. Basi akasema, “Ni—nimefundishwa *hili*. Nami kamwe siwezi kulielewa.” Naye alikuwa ni seremala.

47 Nikaenda nyumbani pamoja naye, usiku mmoja, naye akasema, “Nakwambia. Wakati Norma na hao wengine wakienda ghorofani,” kasema, “hebu—hebu tupate mlo tule. Tukachukua ugali na maziwa ya mtindi.” Hicho ni kitamu kweli. Na kwa hiyo sisi... Ningeweza kukitendea haki sasa hivi.

48 Sijakuwa nikila kwa yapata majuma matatu hapa, kidogo tu, mara kwa mara, kusudi nipate kuwa katika hali nzuri zaidi kwa ajili ya Bwana wangu.

49 Na sasa, tukapata bilauri kubwa ya maziwa ya mtindi baridi kutoka kwenye nyumba ya springi, na kipande kikubwa cha ugali baridi wa mahindi. Basi tukaketi, na kumeng’anya ugali huu wa mahindi mle ndani, tulikuwa tukila. Naye akasema, “Billy, kamwe silielewi Hilo ambalo unazungumzia.”

50 Kwa hiyo, sisi—sisi tukaenda kulala. Yapata, usiku sana, yeye... Tulizungumza mpaka karibu saa saba. Nikashikwa na usingizi mbele yake. Kisha a—akaamka, naye akasema, “Ni—niliota ya kwamba nilikuwa nikijenga jengo huko—huko New Albany, naye mtu huyo akaniachia ramani. Akaenda Florida. Naye alikuwa, kwenye ramani hii, alikuwa na dirisha la kutokeza nje. Nami nikasema, ‘Mtu huyo habitaji dirisha la kutokeza nje huko,’ kwa hiyo nikaliacha tu. Kisha akasema,

“Mtu huyo aliporudi, alisema, ‘Sitakulipa kwa ajili ya jengo hili mpaka utakapolibomoa na kulijenga kulingana na ramani hii.’”

⁵¹ Nikasema, “Kuna kijito papa hapa chini. Hakiko mbali sana. Kwa hiyo, hutaki kwenda ukirarua kitu mwishoni mwa safari. Huenda usiwe na wakati.”

Akasema, “Ni sawa nikiwa nimevaa pajama yangu?”

Nikasema, “Pamoja na yangu, pia. Hebu twende.” Kwa hiyo tukashuka.

⁵² Kwa hiyo binti yake akawa maarufu sana, sana, na wajukuu wake, katika kuimba.

⁵³ Na wao—wao walikuwa ni Ndugu wa United. Binti yake ameolewa, mhudumu wa Ndugu wa United, ama mwana wa mhudumu. Naye mvulana huyu, jamaa mzuri, alikuwa ni mtengenezaji mitambo kwenye kiwanda cha mitumbwi. Naye maskini msichana huyo akijaribu kumwishia Kristo. Ikawa ni shinikizo kubwa juu yao.

⁵⁴ Walikuwa ni watoto wenye vipaji sana. Mmoja wao, kwenye umri wa miaka kumi na saba, alikuwa akifundisha muziki. Alikuwa ametaalimika, naye alikuwa ni msichana mwerevu sana.

⁵⁵ Na kwa hiyo maskini jamaa huyu asingeweza kustahimili shinikizo la kuchokozwa, nao wangemwambia alikuwa ni wa mtindo wa kale, na kadhalika. Basi baada ya kitambo kidogo, mtoto huyo akachanganyikiwa.

⁵⁶ Wa—wakampeleka kwa, kile wanachokiita, Mama Yetu wa Amani, hospitali ya Katoliki huko Louisville, apate tiba ya mshtuko. Nao wakampa . . .

⁵⁷ Hakika, huko ni kubahatisha. Iwapo kuna daktari hapa, natumaini sikuudhi kwa hilo. Lakini wakati mwingine huwafanya wabaya kuliko mwanzoni.

⁵⁸ Na kwa hiyo wakampa tiba ya mshtuko, nayo ikamfanya mtoto huyo kuwa hali mbaya zaidi. Kwa hiyo wakampeleka nyumbani. Majuma machache, iliwabidi kumrudisha tena, na kweli alikuwa katika hali mbaya sana wakati huo. Kwa hiyo wakamweka, na kujaribu kumtibu kule, kwa muda mrefu, naye akazidi kuwa katika hali mbaya.

⁵⁹ Basi siku tatu kutoka wakati huo, walikuwa wampeleke Madison. Hiyo ni hospitali ya wendawazimu ambako wana—wanawaweka kwenye vyumba vya kuta vilivyowekwa vitu vyororo, tangu hapo.

⁶⁰ Kwa hiyo mama akasema, “Hatujashindwa.” Naye akasema, “Tutaona kama tunaweza kumpata Ndugu Branham aje huku akamwombe, kama yuko nyumbani.”

61 Kwa hiyo wakapiga simu, na ikatokea kwamba nilikuwa nyumbani. Kwa hiyo akaja kuniona, kasema, “Ndugu Branham, utaenda kule, ukamwombee?”

Nikasema, “Hakika.”

62 Kwa hiyo akampigia daktari simu. Naye daktari akasema, “Alikuwa nani huyo anayekuja?” Kwa hiyo akamwambia ilikuwa ni mimi. Naye akasema, “Vema, nitakwambia, ngoja.” Kasema, “Tuta—tutaninii. . . Wewe nipigie simu tena, alasiri ya leo.”

63 Vema, akampigia simu, na kuendelea mpaka saa saba usiku. Mke wake akaendelea kusema, “Hayuko.” Kesho yake asubuhi akampigia. “Hayuko.” Basi siku ya tatu walikuwa wamwondoshe mtoto huyo.

64 Kwa hiyo, na—nachukia kusema hili, bali ninayo njia ya kujua. Huyo daktari alikuwa tu akikwepa jambo hilo. Mnaona? Kwa hiyo basi baba alikuwa na wasiwasi kweli. Ilibidi niondoke kesho yake, kuondoka. Hiyo siku ndiyo tu tuliyokuwa nayo.

65 Kwa hiyo mama na baba, na hao dada wengine wawili, wakaja, wakilia, kasema, “Yeye, yeye anakwepa tu.”

66 Nikasema, “Hakika, anakwepa. Lakini hebu niwaambie kitu. Msiseme mimi ni mhudumu. Acheni niende tu kama rafiki, anayeambatana tu nanyi.”

67 Kwa hiyo tukaenda kwenye hospitali hiyo. Mwajua, wanaifunga milango nyuma yako, na kukupandisha kwa lifti ya vipandio, kisha wanaifunga hiyo lifti ya vipandio. Kwa hiyo . . . Naye huyu sista alikuwa akitupandisha.

68 Basi tukaingia kwenye chumba hicho, tukaketi chini kando ya kitanda. Na pale huyo msichana mrembo sana, mwenye umri wa kama miaka kumi na sita na kitu, ameketi pale, amekwisha kabisa. Wewe . . . Yeye, amekodoa macho tu. Ungeweza kupunga mikono yako, naye hata asingeiona.

69 Ndipo nikamwambia, “Ruthie, u—unanikumbuka mimi?” Nikasema, “Mimi—mimi—mimi ni Ndugu Branham.” Nikasema, “Ulizoea kuniita Ndu’ku Bill.” Nikasema, “Ni—nilikukabidhi kwa Kristo, kwenye kitanda cha mtoto. Kwani hunikumbuki?”

70 Anasimama tu na kutazama. Loo, msichana mrembo; nao hao watatu, walikuwa ni utatu, dada watatu. Nami nilijaribu kuuvutia usikivu wake, wala ni—nisingeweza. Alikuwa amekodoa macho. Alikuwa tu amekwisha.

71 Basi nikaketi pale. Nami . . . Hawakuwa na nguzo kitandani katika mahali hapo, mwajua, kusudi wasijidhuru. Basi nikaketi upande wa pili, miguuni mwa kitanda. Mama aliketi, upande huo mwingine wa kitanda hicho kidogo, maskini kitanda hiki kidogo cha mtu mmoja, katika chumba hiki kidogo. Naye msichana huyu alikuwa ameketi kwenye maskini kitu kidogo, kama kiti kilichojengwa ukutani. Naye dada alikuwa

amesimama, na baba alikuwa amesimama karibu na msichana huyo.

⁷² Naye mama alikuwa amesimama pale, huku machozi yakitiririka kutoka mashavuni mwake. Akasema, “Unaona, Billy? Tunaweza—tunaweza kufanya nini?”

Nikasema, “Vema, sikiliza, Norma. Kristo angali ni Kristo.” Mnaona?

⁷³ Akasema, “Hii ilikuwa ndiyo nafasi yetu ya mwisho.” Kasema, “Wakimpeleka kule, mnajua litakalotukia.” Kasema, “Kamwe hatutamwona, nadhani, tena. Na tukimwona, mnajua jinsi, ma—matibabu wanayopata kule.”

⁷⁴ Ndipo nikasema, “Vema, Norma, hebu tusihamaki.” Nikasema, “Tuninii—tungojee tu dakika chache.” Ndipo basi, si zaidi ya niliposema hivyo, huyo hapo msichana huyo amesimama mbele zangu, katika ono, mzima kabisa, akitabasamu. Naye alikuwa akimwangukia kijana mwanamume. Nami nikamwangukia kijana huyo.

⁷⁵ Nikaangukia nyuma. Ono likaniacha. Nikasema, “Norma, hivi yeye ana rafiki mvulana, kidogo ni mrefu na mwenye nywele nyeusi?”

“Naam.”

Nikasema, “Yeye hufanya jambo fulani pamoja nao wakiimba?”

Kasema, “Naam. Hiyo ni kweli.”

⁷⁶ Nikasema, “Msiwe na wasiwasi. Ninayo BWANA ASEMA HIVI. Atapona.”

⁷⁷ Norma akaitupa mikono yake na kunishika gotini, akaangukia juu kwa mumewe, akasema, “Mpenzi, kamwe halikosei.” Kasema, “Kamwe halikosei.”

⁷⁸ Msichana huyo hakubadilika hata kidogo. Nikasema, “Vema, Norma. Unajua ya kwamba nisingaliwaambia hilo sasa isipokuwa niwe nimeliona. Naye Mungu hawezi kusema uongo.” Mnaona? Nikatoka nje ya hospitali na kuingia kwenye gari langu mwenyewe. Wao wakabaki.

⁷⁹ Ndipo yapata saa mbili tangu hapo, simu ilikuwa tu ikilia, nilipokuja kutoka kwa Bw. Wood, huko chini. Na ilikuwa ni baba yake. Alikuwa kwenye simu. Akasema, “Ndugu Branham, ninalo jambo la kukwambia.” Kasema, “Hukuwa umeondoka dakika ishirini, kabla hajarudia fahamu zake, mzima. Naye amechunguzwa na kundi lote la madaktari. Tunampeleka nyumbani asubuhi.”

⁸⁰ Na sasa, mnaona, sasa yeye huimba maskanini sasa. Sasa, wapo wanaume na wanawake hapa, kutoka—kutoka Jeffersonville kule, wanaojua ya kwamba hadithi hiyo ni kweli. Ikiwa mpo hapa ndani alasiri ya leo, inueni mikono yenu, ni

wangapi wanaijua hadithi hiyo? Naam. Mnaona? Kote kote, wanaojua ya kwamba ni kweli, kweli kabisa.

⁸¹ Sasa, ilikuwa ni kitu gani? Maskini mama huyo alitumia ono hilo kama—kama yakini, mkataa. Mnaona?

⁸² Inakupasa, kwa kila jambo, inakupasa kuwa na mahali fulani ungeweza kujifungia. Nami daima nimelitumia Neno la Mungu, kwa sababu hakuna nguzo nyingine ya kufungia niijuayo, kuu kama hiyo, kwa sababu, “Mbingu na nchi zote zitapita,” alisema Yesu, “bali Neno Langu halitashindwa.” Ni nguzo ya kufungia ya jinsi gani!

⁸³ Sasa, Paulo alikuwa na maisha yaliyotiwa msingi kwa Kristo. Yeye... Huyo alikuwa, Kristo, alikuwa ndiye yakini ya Paulo.

⁸⁴ Alikuwa—alikuwa ni mwalimu mkuu, Paulo alikuwa. Alifundishwa chini ya Gamalieli. Naye alikuwa ni mwalimu mashuhuri, wake, chini ya dhehebu la msingi wake wa Kifarisayo. Naye alifundishwa, akaelimishwa, na alikuwa na msingi mzuri sana.

⁸⁵ Nafikiri, wakati alipompokea Roho Mtakatifu, na kushuka kwenda Misri kwa miaka mitatu, nafikiri hapana shaka hapo ndipo alipoanza kuyachukua Maandiko na kuyalinganisha na ufunuo aliokuwa amekuwa nao, aone kama Hayo yalikuwa ni ya kweli. Nanyi mwajua kile kitabu mashuhuri, maarufu sana, cha Waebrania, hakuna mwingine angaliweza kukiandika ila Paulo, kwa sababu yeye alijua jinsi, hiyo mifano na mifano ya mifano. Ni somo la kupendeza jinsi gani!

⁸⁶ Na sasa, Paulo alikuwa amekutana na Yesu siku moja. Akakutana na... Akakutana na Yeye, uso kwa uso, kwenye barabara ya Dameski alipokuwa akishuka kwenda kuwatesa Wakristo.

⁸⁷ M—mgomvi mkubwa akitoa vitisho vikubwa, na kufanya mambo dhidi ya Kanisa la Mungu, akifanya maangamizi Yake, hata kuwatesa hata kufa. Ndipo siku moja akishuka kwenda...

⁸⁸ Sababu ya yeye kuwa na maisha haya yaliyotiwa msingi kwa Kristo ni kwa sababu yeye, binafsi, sasa akiyaweka kando mafundisho yake, alikutana na Kristo kibinafsi.

⁸⁹ Na hiyo ndiyo njia pekee utakayopata kumfahamu, ni kukutana na Yeye. Unaona? Sasa, “Kumjua Yeye ni Uzima,” sio hata kulijua Neno Lake, kadiri Hilo linavyoweza kuwa ni zuri. Hata hivyo, huna budi kumjua Yeye. “Kumjua Yeye ni Uzima.”

⁹⁰ Naye Paulo hakuwa amepata ujuzi huu bado. Ndipo akasema, mahali pamoja hapa, “Maisha ninayoishi sasa...” Ilionyesha ya kwamba alikuwa ameishi maisha tofauti, wakati mmoja. Maisha yake yalikuwa yamebadilishwa.

⁹¹ Basi maisha yako yanapobadilishwa, inakufanya ufanye mambo usingeweza kufanya kwa kawaida. Na, inakufanya

kusema mambo usingeweza kusema kwa kawaida, mtu aliye na maisha yenye msingi wa Kristo.

⁹² Mbona, Paulo alisimama moja kwa moja katikati ya watu, hao Wayahudi, na kadhalika. Alikuwa...chembe moja ya woga kwake. Alijua Yeye aliyemwamini. Na yeye—yeye alikuwa na ma—maisha ambayo asingefanya hivyo kamwe, kama asingekuwa amepata kitu fulani kilichokuwa ni cha halisi na kikamtia nanga.

⁹³ Nafikiri, Mkristo yeyote anapaswa kuwa hivyo, kila mwaminio. Kamwe hupaswi...Nafikiri, hasa, wahudumu kamwe hawapaswi kujaribu kuingia mimbarani mpaka wamekutana na Mungu juu ya huo mchanga mtakatifu ambapo hakuna mwanafalsafa anaweza kulielezea vibaya. Ulikutana na Mungu, nawe unajua hilo, wala hakuna kitu kinachoweza kulificha kutoka kwako.

⁹⁴ Sasa, tuna nyakati ambazo tuna usomi mwingi, wala hamna neno dhidi ya hilo. Hilo ni sawa. Lakini, hayo yote ni mazuri. Lakini wewe, kibinafsi, huna budi kukutana na Mungu, kufikia mahali ambapo hakuna mtu anayeweza kuyapindua Maandiko yoyote. Ulikuwa pale. Wewe, wewe ndiwe uliyekutana na Yeye. Ulikuwa na ujuzi wake. Unamjua. Unaona?

⁹⁵ Nafikiri, kila mhudumu, hasa, na kila mwaminio, anapaswa—anapaswa kupachukua mahali hapa, msimamo huu, kukutana na Kristo kwanza, kibinafsi. Nayo inakufanya ufanye mambo, kama—kama nilivyosema, ambayo kwa kawaida usingeyafanya. Inakufanya kusema mambo ambayo kwa kawaida usingeyasema. Hata hivyo, Hicho ni kitu ambacho umetiwa msingi, au kufungwa kwake. Ni kitu ambacho unajua, kama vile Paulo, kwamba wewe—wewe ulikutana na kitu fulani ambacho kilikuwa ni tofauti na kile ulichopata kuona maishani mwako. Mnaona?

⁹⁶ Ni kama tu meli. Mnaona? Meli ina—ina yakini, na yakini ya meli hiyo ni nanga.

⁹⁷ Sasa, meli hiyo inapokuwa kwenye maji yanayorushwarushwa, ambako kwa urahisi inaweza kutupwa kwenye mwamba, ama—ama kupasuliwa; ama kugonga chini, ambapo ma—maji hayana kina cha kutosha; na yale mawimbi makuu, yakija, yataipiga meli hiyo kwa ghafla, na kuipindua.

⁹⁸ Haina budi kuwa na maji yenye kina cha kutosha kuifanya ielea, la sivyo mawimbi yataipindua. Na—nayo meli iliyo na nanga, tani hizo kubwa, nzito mno za—za chuma ambazo inaangusha, za feleji. Nayo inashuka chini, chini, mpaka inafika juu ya sakafu ya bahari, mahali fulani juu ya mlima. Nayo nanga hiyo kubwa inavuta, wakati mawimbi yakiipiga meli, mpaka inachomeka mikuki yake mikubwa ndani ya mwamba. Basi, hapo, hiyo meli ina yakini. Imetiwa nanga. Huenda mawimbi yakairusharusha kote, lakini, hata hivyo, meli hiyo

inaweza kusimama wima kikamilifu, ambapo imetiwa nanga, kwa sababu ni yakini kwake.

⁹⁹ Basi kama Kristo ndiye Yakini yako, umefungamanishwa Kwake kwa njia hiyo, haijalishi mtu yeyote anasema nini, jinsi mateso yanavyokuwa makali, jinsi tufani inavyoonekana kuwa mbaya, jinsi—jinsi inavyoonekana haiwezekani kwake kutukia. Ikiwa jambo fulani limefanyika ndani yako, ambapo, Kristo anakuwa Yakini yako, ama ahadi yoyote katika Biblia inakuwa yakini yako. Ikiwa wewe ni mgonjwa, na—na wewe unaomba upate uponyaji, na kitu fulani kinakuja kwa hiyo, kinaigonga ahadi hiyo katika Biblia, “Nimeipata,” hakuna kitu kitakachokuyumbisha kutoka Kwake.

¹⁰⁰ Mnaikumbuka ile hadithi dakika chache zilizopita, ya maskini yule mama? Lile ono lilikuwa ndilo yakini yake. Alijua kamwe halikuwa limewahi kushindwa, kwa hiyo lilikuwa ni yakini yake. Kama angeweza kumfanya Mungu kujibu na kusema, “Imekwisha,” haijalishi daktari alisema nini, ilikuwa ni yakini. Ilikuwa imetiwa nanga kabisa.

¹⁰¹ Basi mwanamume ama mwanamke, katika falsafa tu ama kujiunga na kanisa, ama kitu kama hicho, bado hujatiwa nanga. Wewe, ungepeleka barua yako kutoka kanisa moja hadi lingine, kutoka mahali pamoja hadi pengine. Lakini kama ukichukua tu Yakini iliyo halisi, Kristo, ujitie nanga katika Huyo. Haileti tofauti yoyote kijacho ama kiendacho, ungali umetiwa nanga.

¹⁰² Basi kile Mkristo anachohitaji leo hii, katika wakati huu wa atomiki, na wakati huu wa mashaka, unahitaji kitu fulani mbali na ujuzi wa kujiunga na kanisa. Unahitaji nanga, yakini, ambayo unaijua. Kwa sababu, makanisa yatashindwa, na watu watashindwa. Lakini Kristo hawezi kushindwa. Yeye, Yeye ndiye—Yeye ndiye Yakini kwa mwaminio. Basi ikiwa Kristo ndiye Yakini yako, umefungwa Kwake. Na ikiwa Yeye ndiye Yakini yako, nawe umefunganishwa Kwake, basi umefunganishwa kwenye Neno.

¹⁰³ Sasa, sasa, Hii inaonyesha kama tuna yakini ya kweli ama hatuna. Mnaona?

¹⁰⁴ Kama unaweza kusoma katika Maandiko hayo, jambo ambalo Kristo ametuchagua ama kutuagiza kufanya; na, kwa sababu ya kuyumbishwa huku na huku, kama mtu fulani angekwambia Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya wanafunzi ama mtu mwingine; na halafu hulishikili Hilo, basi Kristo siye Yakini yako. Mtu huyo aliyekuongoza ukatoka Njiani ndiye yakini yako.

¹⁰⁵ Lakini kama hilo Neno, Kristo, lingali linashikilia, unaona, basi Yeye ndiye Yakini yako. Haitupasi kuacha chochote kituchoche kututoa nje ya njia ya Neno. Mnaona?

¹⁰⁶ Baadhi yao, siku hizi, inaenda kupata wengi kuliko wakati wowote, siku zinavyosonga, kuwa tutawaona watu wenye huu,

kama Yesu alivyosema, “Mfano wa utauwa.” Na inafikia tu kwenye m—mfano. Tumekuwa nao katika Wamethodisti na Wabaptisti, na kadhalika, kwa miaka, na sasa imenyemelea kwenye Wapentekoste. Na kidogo . . .

¹⁰⁷ Wakati Mungu alipompa mtu Roho Mtakatifu, Yeye alimweka huku uso wake umeelekezwa Kalvari, nalo Neno likiwa mbele yake.

¹⁰⁸ Sasa, mizizi midogo itachipuka kutoka kwenye barabara hiyo kuu, iingie na kujizungusha na kujizungusha kwenye mti huo, nawe unawazia haina madhara. Lakini, muda si muda mwajua, imekushikilia sana hata inakuvuta upande mbaya, inakufanya uegemee upande mbaya.

¹⁰⁹ Na vivyo hivyo falsafa na kadhalika zimeingia miongoni mwetu, mpaka zimeanza kutuvuta kuuelekea ulimwengu. Wewe chukua Upanga mkali wa Mungu ukatao kuwili ukate ujiweke huru na kila kitu, na ukae moja kwa moja kwenye hilo Neno, maana Hilo ndilo Mkataa. Hilo ndilo Yakini, kwa kila mwaminio.

¹¹⁰ Na kama mwanamume ama mwanamke amejazwa na Roho Mtakatifu, moyo wako ndani yako utaitikia kila ahadi ya Mungu kwa “amina.” Hiyo ni kweli.

¹¹¹ Sasa, wakati mtu fulani anapokwambia, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa kwa ajili ya wakati mwingine.”

¹¹² Halafu unafungua katika Biblia na kusoma ambapo Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, wakati wote walipochomwa moyoni mwao. Nao wakamwambia, “Waume na ndugu zetu, tufanye nini? Tufanye nini tupate kuokolewa?”

¹¹³ Sasa, kama kujiunga na kanisa kungalikuwa ndiko alikosema, angesema, “Hamna budi kuutafuta ule—ule mwili na—na kujiunga na kanisa.” Vema, mnaona, kulikuwa na ninii . . . hapakuwepo na kitu kama hicho katika siku hiyo.

¹¹⁴ Kwa hiyo yeye aliwapa maagizo halisi ya kile kinachohitajika. Aliwaambia yale hawana budi kufanya, na umbali ule ungeenda. Akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

¹¹⁵ Basi ni umbali gani? Yesu alisema, katika Marko 16, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mnaona? Umbali gani? “Kote ulimwenguni, kwa kila kiumbe,” ndivyo Injili ilivyo. “Na ishara hizi zitafuatana na kila aminiye: katika Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; ama wakashika

nyoka ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.”

¹¹⁶ Sasa, mnaona, huna budi kuipata hiyo yakini, kitu hicho kilicho halisi, ambacho kinakutambulisha pamoja na Kristo na Neno Lake. Naam. Neno ni Kristo. Na huna budi kuwa na hakika kwamba unaweza kusema “amina” kwa hilo Neno, la sivyo yakini yako si sahihi.

¹¹⁷ Umejenga juu ya kanuni fulani ya imani. Unasema, “Loo, ninaamini Kristo, bali siamini Kitu hicho. Na—naamini Kristo, bali siamini *Hili*.” Basi yakini yako si sahihi. Yakini yako iko kwenye baadhi ya kanuni za imani, na si katika Kristo, kwa sababu Kristo ni Neno.

Yeye pia ni kama nyota ya kaskazini, ndivyo Yeye alivyo, kwa mtu aliyepotea.

¹¹⁸ Sasa, mimi huwinda kote ulimwenguni. Nami nimekuwa nyi—nyikani. Na wakati mwingine, moja ya ninii nzuri zaidi. . . Kama unaweza kuangalia juu na unajua mwelekeo wa nyota ya kaskazini, yeye hukuongoza utoke. Basi m—m—mtu baharini, na wakati ame—amepotea, ikiwa tu angeweza kuipata hiyo nyota ya kaskazini, anaweza kujiongoza basi mahali anakoenda. Sasa, hapo ni wakati amepotea, yeye huitafuta nyota ya kaskazini. Sasa, nyota zingine huhama, bali nyota hiyo ya kaskazini hukaa papo hapo katikati ya dunia. Haijalishi dunia inageukia wapi, hiyo nyota ya kaskazini hubaki vile vile. Inaelekeza kaskazini. Ndiyo nyota ya kweli pekee, nasikia, tuliyo nayo, ni hiyo nyota ya kaskazini kabisa. Sasa, hiyo—hiyo hukupa mwelekeo wako.

¹¹⁹ Basi hivyo ndivyo Kristo alivyo kwako. Kama unataka kwenda Mbinguni, kama unataka kuokolewa, kama unataka kujazwa na Roho, kama unataka kuwa kama Kristo, Kristo ndiye Nyota yako ya Kaskazini. Kama umepotea, usijaribu kuchukua kanuni ya imani. Yeye ndiye Nyota yako ya Kaskazini. Ndiye Njia yako. Ndiye Mwelekeo wako.

¹²⁰ Halafu, kama—kama ukimchukua Yeye kama Nyota yako ya Kaskazini, basi hiyo kabisa inamweka Roho Mtakatifu kuwa Dira yako. Amina. Roho Mtakatifu ndiye Dira yako, nayo Dira itaelekeza tu kwenye Nyota ya Kaskazini. Na kama unao ubatizo wa Roho Mtakatifu, unaweza tu kuelekeza kwa Kristo, naye Kristo ni Neno. Hiyo ndiyo njia ya kupata njia yako ya kurudia. Unaona?

¹²¹ Huwezi kuangalia *hapa* juu na kusema, “*Hii* inaangaza. Nyota *hii* inaangaza hapa.” Na baada ya kitambo kidogo iko mahali pengine. Unaona? Inakubidi kufikia mahali ambapo imeimarishwa kabisa.

¹²² Sasa, Kristo akiwa ndiye Nyota ya Kaskazini, nayo Dira daima huelekeza huko. Na kama kweli umeokolewa, kweli, njia pekee unayoweza kuokolewa ni kupitia Kristo. Basi Roho Mtakatifu, akiwa ndiye Dira yako, atakuongoza moja kwa moja

kwenye Neno. Mnaona ninalomaanisha? Sasa, hilo ni zuri sana! Naye Neno na Kristo ni Mmoja. Wote wawili ni mmoja, utu mmoja. “Hapo mwanzo,” Yohana Mtakatifu 1, “alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Kama Yeye ndiye Nyota yako ya Kaskazini, basi anakwa Yakini yako.

¹²³ Hii ni njia ndefu ya mzunguko, kwa yale ninayotaka kusema. Lakini mtalifahamu, labda, lile ninalojaribu kuwaelezea.

¹²⁴ Hapana budi pawe na yakini maishani mwako. Huna budi kuwa nayo mahali fulani, na kila mmoja wenu ana moja. Huwezi kuendelea bila moja. Huna budi kuwa na yakini.

¹²⁵ Kulikuwako na wakati ambapo mwa—mwanamke, neno la—lake kuhusu maadili ya maakuli, hilo lilikuwa ndilo yakini Marekani. Nafikiri jina lake lilikuwa Emily Post, kama sijakosea. Basi lolote alilosema kuhusu maadili ya maakuli, kama alisema inakupasa kula kwa ninii yako... kula njegere zaka kwa—kwa kisu, hilo, ilikuwa ni hilo—hilo tu. Basi. Na ni kwa nini? Na kama alisema katika kula kuku, unamchukua tu kwa—kwa mikono yako na kumla, haijalishi mtu yeyote alikuangaliaje, ulikuwa sahihi kabisa, unaona, kwa sababu huyo alikuwa ndiye yakini. Alikuwa ndiye yakini ya maadili ya maakuli. Hiyo ni kweli. Chochote alichosema mwanamke huyo, basi.

¹²⁶ Kulikuwa na wakati ambapo, Ujerumani, wakati Adolf Hitler alipokuwa ndiye yakini Ujerumani. Haijalishi mtu yeyote alisema nini, Hitler alikuwa ndiye neno la mwisho. Alichosema Hitler, ilibidi kitekelezwe. Hiyo ilikuwa ndiyo njia yake ya kulifanya. Na haijalishi ni wangapi wao walifikiria lolote kulihusu, Hitler alikuwa ndiye neno la mwisho. Alikuwa ndiye yakini.

Kulikuwa na wakati ambapo Mussolini alikuwa yakini ya Urumi.

¹²⁷ Kulikuwa na wakati ambapo Farao alikuwa ndiye yakini ya Misri. Lolote alilosema Farao, ilibidi lifanywe.

¹²⁸ Lakini, mnaona, hao wote walikuwa aina mbaya ya yakini. Walishindwa, kila mmoja wao. Nikisimama huko Misri, sio muda mrefu uliopita, nilikuwa nikiwazia wakati Mafarao walipoketi kwenye viti vyao vya enzi. Na, mwajua, inakubidi kuchimba chini futi ishirini ardhini kupata ambapo viti vyao vya enzi vilikuwa. Mnaona? Loo, hiyo ingekuwa ni yakini ya namna gani! Imeamgamia wala haiko tena. Nao watu waliotegemea yakini ya aina hiyo, wameangamia pamoja nayo, na kutoweka. Kwa nini? Ilikuwa ni ya kutengenezwa na mwanadamu, na chochote kilichotengenezwa na mwanadamu kitaangamia pamoja na mwanadamu.

¹²⁹ Bali kuna yakini isiyoweza kuangamia. Hiyo ni Neno la Milele la Mungu. Kamwe haliwezi kuangamia. Huna budi kudumu na Hilo.

¹³⁰ Sasa, sasa, tunatambua ya kwamba—ya kwamba tuna yakini hapa. Tunatoka nje hapa na kuwa na kesi. Nawe unapata matatizo hapa nje, na unakuwa na kesi hapa mjini. Wanaweza kuifuatilia kupitia mahakama zingine, na kadhalika. Huenda hatimaye ikafikia kwenye Mahakama Kuu. Lakini uamuzi wa Mahakama Kuu ndio yakini. Hiyo ndiyo mwisho wa kesi. Huo ndio umbali wote unaoweza kwenda. Hiyo ndiyo mahakama ya mwisho, ni Mahakama Kuu, na hiyo ni yakini.

¹³¹ Sasa, wakati mwingine hatukubaliani nao, na—na, ama hatuyapendi maamuzi yao. Lakini, vivyo hivyo tu, ni yakini, kwa sababu taifa limefunGANishwa kwake, mnaona, yale Mahakama Kuu isemayo. Haijalishi kama nikisema wamekosea; hilo haliwafanyi kuwa makosani. Katika taifa hili, wao ni sahihi. Chochote uamuzi wao ulicho, ni sahihi. Yakini, hatuna budi kuwa nayo. Kama haikuwapo, mahali fulani, kesi isingeisha kamwe. Lakini kunapaswa kuwe na mahali fulani ambapo kesi hiyo inafikia mwisho wake, na hapo ni katika Mahakama Kuu. Mtu yeyote anajua hilo. Imekwisha ikiisha kupitia kwenye Mahakama Kuu. Wanatoa uamuzi, huo unatosha. Hakuna mwingine. Hakuna mahali pengine unapoweza kwenda maana hiyo ndiyo mahakama yao ya juu kuliko zote. Kuna . . . Hapana budi kuwa na yakini, hapana budi kuwa na yakini kotini.

¹³² Inatubidi kuwa na yakini kwenye mchezo wa mpira. Hivi mlujua hilo? Mchezo wa mpira hauwezi kuendelea vizuri pasipo na yakini, na hiyo ni mwamuzi. Sasa, wakati mwingine ha—hatuyapendi maamuzi yake, bali ni—ni—ni yakini. Yeye ndiye yakini, kwa vyovyote vile. Kama . . . Haijalishi, kama tunataka kusema, na wengine waseme, ya kwamba—ya kwamba ilikuwa goli, ama ilikuwa ni mpira; naye anasema imeingia, hivyo ndivyo ilivyo. Usibishane naye. Yeye yupo hapo. Ndiye yakini katika mchezo huo wa mpira. Kwa sababu, kama alisema, “Goli limeingia,” huwezi kubishana, unaweza ukaitupa kofia yako huko nje, na kulipinga, bali ni goli, kwa vyovyote vile. Amina. Sasa hebu tuwazie kwa dakika moja tu. Vipi kama hapakuwapo na mwamuzi katika huo mchezo? Kungekuwako na ubishi wa namna gani? Ingekuwa ni mchafuko kabisa. M—msingeweza kucheza mchezo pasipokuwako na yakini ndani yake. Michezo haina budi kuwa na yakini.

¹³³ Na kama michezo haina budi kuwa na yakini, vipi kuhusu maisha? Hayana budi kuwa na mahali pa kuegemea. Na kila mwanadamu hapa, alasiri ya leo, una yakini yako mahali fulani, mkataa wako, huo ndio neno la mwisho.

¹³⁴ Tazameni, kungekuwako na ubishi na kila kitu kwenye mchezo huu wa mpira. Wote ungeishia katika machafuko.

¹³⁵ Mwajua, taa nyekundu ni yakini kwa trafiki. Lakini vipi kama taa nyekundu haifanyi kazi? Vipi kama taa nyekundu imezima unapofika pale? Mmoja aseme, “Ni—ni—nilifika hapa kwanza.” Huyu mwingine aseme, “Nina haraka kwenda kazini.” Nena kuhusu msongamano wa magari!

¹³⁶ Hiyo ni karibu shida tuliyo nayo na makanisa yetu na kadhalika. Ni msongamano kwelikweli! Taa nyekundu lazima imezimika, mahali fulani.

¹³⁷ Loo, ugomvi na ubishi, mbona, kamwe msingeweza kuumaliza. Hapana budi pawe na kitu fulani pale, kusema, “Wewe nenda, na *wewe* ngojea,” na kadhalika, la sivyo sote tungekuwa na vurugu.

¹³⁸ Vema, sasa, katika imani zetu, katika madhehebu yetu mia sita na kitu mbalimbali. Naam. Nafikiri ni mia tisa sasa, ya—ya madhehebu mbalimbali. Hapana budi pawe na yakini mahali fulani. Kama Katoliki ni ya kweli, Protestanti imekosea. Kama Methodist ni ya kweli, Baptisti imekosea. Kama Pentekoste ni ya kweli, basi hao wengine wamekosea. Na—na hapana budi pawe na kitu fulani mahali fulani. Nawe utaliwekea msingi namna gani, usipochukua Yakini ya Mungu? Hiyo ni Kristo.

¹³⁹ Naye Yesu alisema, katika Yohana 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Ni jambo la yakini kwamba Kristo aliahidi hilo. Hilo ni Neno Lake. Hatuna budi kuliadini hilo. Kasema, “Yeye . . .”

¹⁴⁰ Katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 5, kifungu cha 24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Hiyo ni yakini. Jambo ndilo hilo. Sasa, si yeye ajifanyaye anaamini, bali, “Yeye aaminiye.” Mnaona?

¹⁴¹ Sasa, hatuna budi kuwa na yakini, na Yeye ndiye hiyo Yakini. Na Yeye na Neno Lake ni sawa. Hatuwezi kuwatenganisha. Naam.

¹⁴² Kama taa nyekundu ilikuwa imezima, tungekuwa na msongamano wa magari, loo, jamani, mbaya, pia. Hapana budi pawe na yakini.

¹⁴³ Na kwa hiyo, mnajua, imekuwa hivyo siku hizi, haidhuru, shida yake ni kwamba, ni kile kilichotufikisha kwenye msongamano huu mkubwa wa magari tulioingia. Kidogo ni njia fidhuli ya kulielezea, bali hata hivyo mnajua yale ninayotaribu kusema.

¹⁴⁴ Angalieni. Sababu ya sisi kuingia mle ni kwa sababu kwamba kila mmoja wetu anajitengenezea yakini yetu wenyewe. Mnaona? Tuna yakini yetu wenyewe. Kila kanisa lina yakini yake. Kila kundi lina yakini yake. Nao wanasema, kila mmoja wao, alisema, “Sisi ndio Kweli, njia. Tunayo yote. Hamna

uhusiano wowote na Hiyo. Ninyi mko katika uchache. Sisi, sisi ndio kundi lililo kubwa kuliko yote.” Nao watu hufanya hivyo. Hiyo ni . . . Hampaswi kufanya hivyo.

¹⁴⁵ Mpaka, ni karibu kama ilivyokuwa, siku za Waamuzi, ambapo, “kila mtu anafanya yaliyo mema machoni pake.” Mnaona? Anawazia, machoni pake mwenyewe, anafanya. Lakini, wao, huwezi kufanya hivyo. Kuna njia nyingi mno mbalimbali. Mnaona? Na kwa kweli kuna Njia moja pekee, na Kristo ndiye Njia hiyo. Naye Kristo na Neno Lake ni kitu kile kile. Sasa, mnaona, hamna budi kuwa na Kitu fulani tunachoweza kukikaribia na kusema, “Hiki Ndicho,” na kinaweza kuthibitishwa ya kwamba ndivyo kilivyo, hivyo ndivyo kilivyo, mnaona, Yeye.

¹⁴⁶ Katika siku za waamuzi, sababu kila mtu alifanya machoni pake mwenyewe kile alichodhani ni sahihi, ni kwa kuwa, katika siku hizo, “Neno la Mungu lilikuwa adimu. Hawakuwa na Hilo.” Pia, manabii, hawakuwako. Hakukuwako na manabii katika siku hizo, kusimama kwenye Neno na kuwaongoza Israeli. Kwa hiyo, Neno halikuwa likija, kwa hiyo kila mtu alifanya aliyoyaona kuwa ni mema machoni pake mwenyewe.

¹⁴⁷ Na hapo karibu ndipo tumefikia tena siku hizi, ndugu zangu. Mnaona? Kila mtu machoni pake mwenyewe, asema, “Vema, sasa, kama ninataka kuchukua kanuni muhimu! Kama ninataka kufanya *hiki*, ama dini fulani! Ni—ni—ninaamini, dini yangu, ni kufanya *hivi-na-hivi*.” Na wewe—wewe unaona hilo. Kila mtu anaona hilo.

¹⁴⁸ Wanawazia, “Vema, ni—ninaenda kwenye shule ya Jumapili Jumapili asubuhi. Mimi ni mzuri kama yeyote mwingine.” Vema, hilo, hilo ni jema. Ungali ungeweza kwenda, uende kwenye shule ya Jumapili na—na uwe mwema, hilo ni sawa. Bali kama huna kitu fulani zaidi kidogo kuliko kuhudhuria shule ya Jumapili!

¹⁴⁹ Mtu fulani alisema, “Mimi huzishika zile amri kumi.” Mmoja anaweka siku ya sabato. Huyu mwingine anafanya jambo lingine. Na, hata hivyo, tumefikia mahali hata kila mtu anawazia, vema, wanafanya tu yale wanayofikiria ni sahihi. Lakini hilo haliyafanyi kuwa sahihi. Si kwa njia zozote, haliyafanyi. Tutaona hilo katika dakika chache, mnaona, ya kwamba haliyafanyi kuwa sahihi.

Mungu anayo njia.

¹⁵⁰ Biblia ilisema, “Iko njia ione kanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.” Na hakuna mtu anayetaka kufa. Huo ni utengano. Hatutaki kutenganishwa na Mungu. Wala hatutaki . . .

¹⁵¹ Tunataka kuishi. Maisha ndiyo hazina iliyo kuu kuliko zote ambayo—ambayo mwanadamu anaweza kuwa nayo. Na sasa hatuna budi kutafuta kujua Uzima ni kitu gani. Na Yeye alisema,

“Neno Langu ni Uzima.” Huo ndio Uzima unaopaswa kuwa nao, Neno likiishi ndani yako.

¹⁵² Sasa angalieni. Niliona hili katika wongofu wangu wa mwanzoni, nilipokuwa tu ni mvulana. Niliona hilo. Nami nilijua ya kwamba nilihitaji yakini. Kwa hiyo nikalisoma Neno la Mungu, nami nikaona ya kwamba Neno hili lilikuwa ni Kristo. Na mimi—mimi nilitaka Hilo liwe Yakini yangu. Kwa hiyo nikaliamini Neno Lake. Ndipo nikamsikia akisema, Mle ndani, “Ukikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yako, unaweza kuomba utakacho nawe utapewa.” Sasa, ni ahadi ya jinsi gani!

¹⁵³ Sasa, tuko wapi leo hii, ndugu zangu? Tuko wapi? “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, basi mnaweza kuomba mtakalo nanyi mtatendewa.” Sasa, Hilo, hilo ni Neno la Kristo Mwenyewe. Lakini, kitu gani? Neno halina budi kukaa ndani yako. “Mkikaa ndani Yangu, katika Kristo, na Neno Langu ndani yenu.” Basi, tunaingiaje katika Kristo? Kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Basi, hiyo ni sehemu moja. Lakini, basi, “Mkikaa ndani Yangu, halafu basi Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi mnaweza kuomba mtakalo.” Lakini hamna budi kuwa na yote mawili, Kristo na Neno. Na kweli huwezi kuwa na Moja bila hilo Lingine, hiyo ni kweli, kwa sababu ni Kitu kile kile.

¹⁵⁴ Huwezi kuwa na Baba bila kuwa na Mwana. Huwezi kuwa na Mwana pasipo kuwa na Roho Mtakatifu. Ni Roho Yule yule.

¹⁵⁵ Kwa hiyo, basi, unaona, hu—huwezi—huwezi kulifanya kwa njia nyingine yoyote kuliko kuichukua Yakini iliyotolewa na Mungu kwa ajili ya maisha yetu. Sasa mimi nimefunganishwa Kwake, kwa Neno Lake. Yeye ndiye Yakini yangu. Nami nimeona kwamba ni jambo kuu na la thamani ku—kumwishia Yeye.

¹⁵⁶ Sasa, makanisa mengi. . . Hebu nizungumze tu juu ya yakini. Kwa kanisa Katoliki, papa ndiye yakini yao. Na haidhuru kile kijacho, kile kiendacho, kile mtu mwingine asemacho, kile Biblia isemacho, hicho hakimaanishi kitu.

¹⁵⁷ Nilikuwa na mjadala sio muda mrefu uliopita pamoja na kasisi. Alikuwa kuniuliza kuhusu. . . Nilimbatiza msichana mdogo. Naye alikuwa ameolewa na mvulana Mkatoliki, alikuwa akigeuka kuwa Mkatoliki. Basi akaniuliza jinsi nilivyombatiza, nami nikamwambia. Ndipo tukaanza kuzungumza juu yake. Ndipo akasema, “Wajua, kanisa katoliki lilikuwa likibatiza kwa kuzamisha, namna hiyo.”

Nikasema, “Lini?”

Naye akasema, “Huko nyuma katika siku za Biblia.”

¹⁵⁸ Nikasema, “Unamaanisha ya kwamba unaamini ya kwamba Wakristo wa mwanzoni, kama vile Petro, Yakobo, na Yohana, na hao wengine, walikuwa ni wakatoliki?”

Akasema, “Ndivyo walivyokuwa.”

¹⁵⁹ Nikasema, “Basi mimi ni mkatoliki zaidi ya ulivyo wewe.” Nikasema, “Mimi ni wa katoliki ya mtindo wa kale, unaona, si yule ambaye—ambaye anachukua mwelekeo huu mpya wa lile wafanyalo siku hizi, na kuuita dini.”

¹⁶⁰ “Vema,” yeye akasema, “unaona, Mungu alimpa Petro nguvu Zake, na—na hilo ni kanisa. Na ninii. . . Mungu yuko ndani ya kanisa Lake.”

¹⁶¹ Nikasema, “Hakuna Maandiko katika Biblia, kusema hilo. Hakuna ahadi inayosema hilo. Biblia ilisema, ‘Mungu yuko katika Neno.’ Kweli.

¹⁶² Mungu yuko katika Neno. Neno ni kweli. Nami niliona mle katika Biblia ambapo ilisema, ya kwamba, “Yeye atakayeongeza neno moja Kwake, ama kuondoa Neno moja Kwake, huyo ataondolewa, sehemu yake, kutoka kwenye Kitabu cha Uzima.” Sasa, nilijua hiyo ilikuwa ni Yakini, ya kwamba Neno hilo lisingeweza kubadilika, kwa hiyo nikaikubali Hiyo. Nikasema, “Sasa, Bwana, hebu nilifiche moyoni mwangu, kwamba nitaliweka Hilo na kuwa na kicho Nalo. Na hata iwe nini, nitatembea, na Wewe uniongoze.” Na Hilo limekuwa Yakini yangu.

¹⁶³ Sasa, kwa kanisa la Kiprotestanti, mara nyingi, katika dayosisi, neno la askofu, ingawa ni kinyume na Neno la Mungu, linakuwa ni yakini kwa kundi hilo la Wakristo. Haijalishi Neno linasema nini, kama askofu akisema *hivyo*, hilo latosha, askofu mkuu wa Canterbury. Haijalishi nini, Wa—Waingereza wanaokwenda kwenye kanisa hili la Kianglikana, haijalishi watawazia nini, kama askofu mkuu akisema kitu *fulani*, hicho ndicho.

“Aa,” unasema, “hilo ni baya sana.”

¹⁶⁴ Lakini, unajua, sasa, ngoja kidogo. Tunaweza kushuka chini kuja moja kwa moja nyumbani kwa Pentekoste kama mngetaka. Hakika unaweza. Lakini na—natumaini tu mtafika pembeni na kuona yale ninayomaanisha. Mnaona?

¹⁶⁵ Mnasema, “Huyu hapa ndugu aliyejazwa na Roho Mtakatifu, na, yeye, Bwana anatenda kazi pamoja naye.”

¹⁶⁶ “Vema, nenda ukamuulize kiongozi kama tunaweza, kwanza, kama tunaweza kuwa na yeye. Yeye ana kadi ya namna gani?” Mnaona, hiyo ndiyo yakini basi kwa kanisa hilo. Hiyo ni kweli. Huenda tukasema “amina” kuhusu Wakatoliki na kuhusu Wa—Wa—Wapresbiteri, na kadhalika, lakini vipi kuhusu—kuhusu wakati inapofikia nyumbani? Mnaona? Tuna ninii. . . tuna yakini bandia.

¹⁶⁷ Hakuna kitu kilicho juu zaidi katika Biblia, katika kanisa, kuliko mzee wa kanisa hilo. Ni kanisa linalojitawala, naye Roho

Mtakatifu anafanya kazi katika njia yoyote atakayo Yeye. Yeye huishi miongoni mwa watu Wake.

¹⁶⁸ Lakini tuna yakini nyingine, mwangalizi mkuu mahali fulani, anayetuambia la kufanya. Na ikiwa haliambatani na kile wanachowazia, ama kitu kama hicho, basi, “Hilo halikubaliki. Hilo si la Mungu.” Loo, jamani! Ni jambo baya jinsi gani! Ni tatizo la aina gani tumeingia! Si ajabu tuko hapa nje tukililia uamsho. Nayo anga imejaa nguvu za Kipentekoste, na sisi hatuwezi kuzifikia. Hiyo ni kweli. Ni kwa sababu tumeikataa Yakini ya Mungu. Kweli.

¹⁶⁹ Ufunuo wa Kristo, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.” Ni Yakini. Nalo Neno la Mungu ndilo Yakini Yake. “Mwili na damu havijakufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia jambo hili. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.” Mnaona? Yakini halisi!

¹⁷⁰ Lakini, mnaona, tunachukua kitu kingine kama yakini. Kama dhehebu letu likinena dhidi ya Neno, basi unachukua neno la dhehebu hilo kwa ajili yake. Hupaswi kufanya hivyo. Ninajaribu kujiweka dhahiri, katika misimamo yangu. Nami . . . Kumalizika kwa mkutano huu, ninajaribu kuwaambia sababu ya mimi kutenda na kusema mambo niliyosema, kwa sababu muda mrefu uliopita nilimchukua Kristo kama Yakini yangu.

¹⁷¹ Kanisa la kwanza nililojiunga nalo lilikuwa ni kanisa la Kibaptisti, nami ninawapenda ndugu hao. Walikuwa ni wazuri. Lakini, ilipofikia mahali ambapo ilinibidi kufanya jambo fulani ambalo lilikuwa ni kinyume na Maandiko haya, Neno la Mungu lilikuwa kwanza, kwa sababu nilikuwa nimefunanganishwa kwenye Neno hilo. Kweli. Sina neno dhidi . . . Wakati Dk. Davis aliponijia na alitaka mimi nifanye jambo fulani pale ambalo kabisa lilikuwa ni kinyume na maandiko, nami nikampelekea, yeye alisema, “Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya kizazi kingine, sio la hiki.”

¹⁷² Nikasema, “Mimi nimefunanganishwa na Neno. ‘Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe Kweli.’”

¹⁷³ Hiyo ilikuwa ndiyo Yakini yangu. Na kutoka . . . Hiyo imekuwa ni miaka thelathini iliyopita, ama zaidi, nami ningali kwenye Neno lilo hilo. Na hapo ninataka kuishi na kufia, Hilo likiwa ndilo Yakini yangu. Juu ya hali hiyo ninamkubali Kristo.

¹⁷⁴ Na sasa, sio kwa sababu kwamba ni wewe unayetaka kuwa tofauti. Si kwa sababu . . . Maana, juma hili, nimesema mambo ya kuchoma sana. Na kama nilifanya hilo kusudi tu niwe tofauti, basi ninahitaji kwenda kwenye Yakini, mimi . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Na—nahitaji to—toba madhabahuni. Lakini mngewezaje kuniita nikatubu, nami nimewaambia Kweli? Hiyo ni kweli. Naye Mungu ameliunga mkono na

kuonyesha lilikuwa ni Kweli, kwa Neno, nalo Neno ni hai. Mnaona? Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁷⁵ Sasa, hiyo ndiyo sababu nimesema, na kufanya mambo nifanyayo. Huenda likawa kinyume na madhehebu yetu mbalimbali na mifumo. Si kwa sababu ninataka kuchukua upande na mtu mmoja, ama kuchukua upande na huyo mwingine. Kwa sababu, nilijitolea kabisa kwa kitu kimoja.

¹⁷⁶ Nilipookoka, ama Kristo alipoanza kutenda kazi moyoni mwangu, nilishuka kwenye kanisa Katoliki, maana watu wangu, Waairishi na Katoliki. Nami nikaona jinsi alivyolisema hilo; halikusikika sawa. Basi nilihama-hama mahali hadi mahali. Ndipo hatimaye, yeye akasema, “Mungu yuko ndani ya kanisa Lake.”

¹⁷⁷ Vema, kama Mungu yuko ndani ya kanisa Lake, ni kanisa gani hilo? Hapa... Vema, wao wanasema, “Ni—ni kanisa letu.” Vema, ni lipi kati ya makanisa Katoliki? Kumbukeni, yote yamevunjika, pia. Naam, bwana, yote ni tofauti. Mengine huoa, na mengine hayaoi, na mengine ya Kiyunani, mengine Othodoksi, na, vema, kuna aina tu mbalimbali, Kirumi. Mengine yanamkubali papa, na mengine hayamkubali. Mnaona, yamevunjikavunjika, pia. Ni lipi kati ya makanisa hayo, basi, lililo sahihi? Unaweza kuweka wapi imani yoyote? Kama wewe ni Mkatoliki, na unaliadini kanisa, basi ni kanisa lipi? Ni lipi kati ya makanisa yenu ya Katoliki?

¹⁷⁸ Kama wewe ni Mprotestanti, unasema, “Vema, vema, ni lipi—ni lipi lililo la kweli? Methodisti, Baptisti, Lutheri, Presbiteri, vema, ni lipi lililo sahihi?”

¹⁷⁹ Mungu yu sahihi. Neno Lake ni sahihi. Wengine si sahihi. Kama ni... Hiyo ni sahihi mradi tu wanadumu pamoja na Neno. Lakini unapoliacha Neno, basi umemwacha Mungu. Maana, Mungu analiangalia Neno Lake, kulithibitisha. Hana budi kulifanya halisi. Hana budi kulifanya litende kazi. Hiyo ndiyo sababu ninyi watu mna njaa ya uamsho. Ni wakati wa vitu hivi kuwa hapa. Kama mliwahi kuniamini kujua kile nilichokuwa nikizungumzia, ninyi kubalini hilo. Ile saa imewadia sasa.

¹⁸⁰ Lakini, shida yake ni kwamba, tunazo yakini nyingi sana, hatujui mahali tulipofungiwa. Amina.

¹⁸¹ Sasa najisikia wa kidini. Mnaona? Kweli. Ninataka kutoa hilo kwenye mfumo wangu. Kweli.

¹⁸² Tuna vifungo vingi sana, kimoja kikivuta *huku*, na kimoja *huko*, na kimoja dhidi ya kingine. Watu wanajua je la kufanya? Na msukumo wa Roho Mtakatifu anaposhuka, akijaribu kupata mahali pa kujiingiza Mwenyewe, apate kutenda kazi, Neno kwa Neno, Neno kwa Neno.

¹⁸³ Sasa, ninyi watu wa Kipentekoste mnaamini, wakati karama zinapoanza kurudi kanisani, juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu,

na kunena kwa lugha, nanyi mlikaa moja kwa moja pamoja na hilo. Mliamini hilo. Sasa, hilo ni sawa. Lakini kwa nini mnasimama hapo? Mnaona? Kwa nini mlisimama hapo?

¹⁸⁴ Wakati Israeli walipokuwa safarini kwenda kwenye nchi ya ahadi, na wakati waliposimama nyikani, walikaa huko kwa muda wa miaka arobaini; na safari tu ya siku moja kutoka kwenye kila ahadi, nchi yote, kamilifu ya ahadi.

¹⁸⁵ Nao Wapentekoste, wakati walipovuka, wakicheza na kupiga makelele kama Miriamu na hao wengine, walipofika huko nyikani, walifanya jambo lile lile ambalo Musa alifanya . . . ama sio . . . Israeli walilofanya. Walitaka sheria. Neema ilikuwa imewapa kila kitu tayari. Walitaka kitu fulani kusudi waweze kuwa na madaktari, na ma-Ph.D, na ma-LL.D, nao wakayapata. Nao wakasafiri kule mpaka kila mmoja wao akafa. Kweli.

¹⁸⁶ Ndipo Mungu akawachukua watu wawili na kuwatuma huko: Kalebu na Yoshua. Mbona, walikuwa yapata tu—yapata tu maili arobaini ya safari, ndiyo tu iliwabidi kutembea. Mbona, walikuwa umbali wa siku moja ama mbili tu kutoka kwake. Lakini walingojea hapa nyuma miaka arobaini, mpaka wakaondoa upuuzi huo wote kutoka kwao, mpaka hao watu wote wakafa.

¹⁸⁷ Vema, ni karibu wakati wa mabadiliko sasa. Tu—tulianza kuunda madhehebu, kufanya jambo lile lile tulilotoka kwake, na kulirudisha moja kwa moja nyuma, na kufanya *hii* nguzo ya kufungia, na *hii* yakini. “Na kama hawaliamini Hilo kabisa kwa njia *hii*, Mungu ahimidiwe, hata hawako ndani Yake hata kidogo.” Kwa hiyo mmefanya nini? Kuketi kitako na kupata wafuasi.

¹⁸⁸ Nao wafuasi wanajua nini? Wanageuka kwenye Neno la Mungu, nao wanaona jambo fulani likitukia, ambalo ni Neno la Mungu hasa, mbona, hawajui waelekee wapi. Wanaenda kumwuliza askofu fulani ama kiongozi fulani, “Ni kitu gani *hiki*, na ni kitu gani *kile*?”

¹⁸⁹ Mbona, inanikumbusha juu ya kundi la kuku wa kianguilio. Daima nilimhurumia kuku wa kianguilio. Yeye, angefanya “chi, chi,” huku hana mama wa kumwendea. Yeye alianguiliwa kwa mtambo.

¹⁹⁰ Hivyo ndivyo wengi wa hawa wahubiri katika siku hizi: walianguiliwa kwa mtambo mkubwa. Wakipiga makelele kumhusu Mungu, wala hata hawajui Kitu hicho ni nini. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹¹ Yeye alikuwa kikamilifu. Alikuwa amefunganishwa kwa Mungu, naye Mungu alikuwa ni Neno, ndipo Mungu akalithibitisha hilo kupitia Kwake. Mnaona? Lakini sisi hapa leo hii. Mnaona? Tuna yakini nyingi kupita kiasi, wala si yakini sahihi. Mnaona? Ipo Njia moja tu, nayo ni Yesu. Yesu alisema, “Mimi ndimi Njia.” Na Yesu na Neno ni kitu kile kile.

¹⁹² Na sasa Mungu ametabiri katika siku hizi za mwisho, juu ya yale yatakayokuja kutokea. Yeye aliahidi mambo haya katika siku za mwisho. Yesu aliyaahidi, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Maandiko yote Yeye alioahidi kwa ajili ya siku za mwisho, nasi tunaishi moja kwa moja katika wakati huo. Naye Mungu, Roho Mtakatifu, anatenda kazi juu ya watu.

¹⁹³ Na jambo pekee mnalotaka kufanya ni kucheza katika Roho na kunena kwa lugha. Hayo tu ndiyo mjuayo. Hayo tu, mbegu, imepandwa. Tunachohitaji ni Injili kamili kupandwa katika moyo wote, kwa nguvu kamili, kuleta yakini kamili. Kuna nini?

¹⁹⁴ Hivi mlipata kuwazia yale Israeli waliyofanya kule nyikani? Walioa wake. Waliwalea watoto, na mimea, na kadhalika, wakawabusu watoto wachanga, na kuzika wafu, na kuwaoza vijana. Mungu aliwabariki na walifanikiwa, lakini wangali walikuwa nje ya nchi ya ahadi.

¹⁹⁵ Na hivyo ndivyo Pentekoste ilivyo leo hii. Miaka arobaini iliyopita, usingeweza kuwazia ulikuwa... Mama na baba yako wangelishikwa na mshtuko wa ghafla kama wangeliwazia ungalifikia kwenye hali kama hii. Hakika.

¹⁹⁶ Hao watu wa kale walikuwa wamejifunga kwenye Yakini hiyo, na kulishikilia hilo Neno, haijalishi lilikuwa nini. Hamna dhehebu, viongozi, watu wa wilaya, ama maaskofu, watakaowaambia lolote kulihusu. Walitembea katika Roho, kisha wakatoka na kufanya miujiza na kutenda mambo. Walikuwa na mikutano ya Mtaa wa Azusa ikiendelea kila mahali, mikutano ya vichakani.

¹⁹⁷ Na, vema, hata huwezi kuwatuma watu pembeni mwa mtaa tena kushuhudia. Loo! Mnaona? Tuna kitu gani? Jambo lile lile walilokuwa nalo Israeli.

¹⁹⁸ Sasa, alitokea jamaa pale kwenye wakati wa mwisho, na kuanza kuelekeza, baada ya miaka arobaini, “Kuna nchi nzima iliyojaa baraka huko ng’ambo. Na ninii yote...” Maana, wakati ulikuwa umewadia, ambapo Mungu alikuwa anaenda kuwavusha.

¹⁹⁹ Saa imewadia sasa, ambapo Yeye anataka kulifanya Kanisa tayari. Nitasema hili kwa sauti ya kinabii, natumaini. Silisemi katika Jina la Bwana, bali ninaamini hili ni kweli. Unyakuo, mtakuwa mkizungumza juu ya Unyakuo, wakati Unyakuo umepita, muda mrefu. Naam. Mtakuwa mkisema, “Mungu abarikiwe, Unyakuo unakuja.” Umepita.

Hivi Yesu hakusema kuhusu Yohana?

²⁰⁰ “Kwa nini waandishi wanasema ya kwamba Yohana, kwanza? Ama, alisemaje ya kwamba Eliya hana budi kuja?”

²⁰¹ Akasema, “Amekuja tayari wala hamkujua. Lakini mlifanya vile hasa mlisema yeye angefanya.”

202 Siku moja itatokea hukumu juu ya nchi. Na muda si muda mwajua, mtawaona watu hapa wakiutazamia Unyakuo, nao tayari wameondoka muda mrefu uliopita. Utakuwa ni katika uchache sana. Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu. Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu!”

203 Tunafikiri kundi hili kubwa la chakula cha mzinga hapa, majivu ya atomiki, linaenda. Litaenda tu ikiwa lina Uzima wa Kristo ndani yake, kwa sababu Mungu atalifufua. Hiyo ni kweli.

204 Kutakuwako na Unyakuo. Mnawazia, watu wawili ama watatu *hapa*, na mmoja *huku*. Na mahali pengine, mtu fulani anakosekana, walidhani walitoroka kutoka nyumbani. Hao, afadhali mwe waangalifu, huenda waliondoka. Kuutazamia Unyakuo, nao umepita tayari. Sasa, hilo si kinyume na Neno. La, si kinyume. Yeye alikuja kama mwizi usiku. Mnaona? Watakuwa wameondoka kabla hamjajua hilo.

205 Mungu huweka nguvu Za—Zake kuu Kanisani, wala haiingizi kundi kubwa mno. Inaingiza wachache. “Msiogope, enyi kundi dogo. Ni mapenzi ya Baba yenu...” Ninyi mnaoishikilia Yakini, hiyo ni kweli, pamoja na thibitisho la Mungu akitenda kazi ndani yake.

206 Kwa hiyo, mnaona, tunaishi katika wakati wa kuogofya mno, na huo ndio, huo msukumo uko juu ya kanisa. Vema, mnataka kuona kitu fulani. Mnataka kuona kitu fulani. Lakini, sasa, Mungu anawezaje kuliangalia Neno Lake, kulithibitisha, naye mtu akikataa kuliadini Neno hilo wala hatalipokea moyoni mwao? Jua linawezaje kuiangazia mbegu na kuihuisha, wakati haina uhai wowote ndani yake? Haina budi kuwa ni mbegu iliyorutubishwa. Kwa hiyo, kanuni ya imani inarutubishwa ipate kuleta wafuasi wengi.

207 Lakini Neno linarutubishwa kufanya watakatifu, kufanya waaminio. Hiyo ni kweli. Mungu hutenda kazi kutimiza Maneno Yake. Yeye—Yeye huliangalia, apate kulithibitisha. Naam, bwana.

208 Sasa, sasa, hakika, kanisa Katoliki linachukua nanga yao, nyota yao ya kaskazini, na kwa ajili ya mafanikio yao. Na ni yale papa asemayo, ni yasiyoweza kukosea kwa upande wa Kirumi wa kanisa Katoliki. Waprotestanti, askofu, kanuni fulani ya imani. “Hiyo ni kinyume na kanuni yetu ya imani.” Na baadhi yake inapinga vitu mbalimbali, imani zao za kimadhehebu, na kadhalika.

209 Mwajua, ninajisikia kama vile Paulo alivyosema hapa. Ninaangalia Maandiko katika Matendo 20:24. Yeye alisema, “Sijali lolote la mambo haya.” Amina. Kwa nini? Kwa kuwa alikuwa ametiwa nanga. Alikuwa na yakini. “Tangu nilipokutana na Yeye, nikiwa njiani kwenda Dameski,” kama ningaliweza kuzungumza na Paulo, “Yeye alinigeuza,

akanirudisha nianze kwa njia nzuri. Nilikuwa nimeondoka kwenye Neno. Akanirudisha kwenye Neno.” Naam, bwana.

²¹⁰ Sikilizeni. Ninajisikia hivyo, pia. Ninajisikia ya kwamba mtu yeyote aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, anayempenda Mungu na kulipenda Neno Lake, Mungu analo kusudi katika hilo. Mungu alikuwa na kusudi la kumgeuza Paulo. Hivi Yeye hakusema, “Nitaonyesha ndani yake” utukufu Wake?

²¹¹ Mungu alikuwa na kusudi aliponiokoa mimi. Nimekusudia kufanya mapenzi Yake, “Sio kuongeza Kwake wala kuondoa Kwake.” Ufunuo 22:19 ilisema, “Yeyote atakayefanya hivyo, sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima.”

²¹² Nimedhamiria kutoongeza jambo moja la maoni yangu mwenyewe kwenye hilo Neno. Nimedhamiria kulisoma jinsi tu lilivyo, na—na kumwomba Mungu ya kwamba nitaufungua moyo wangu na kulipokea. “Fanya kazi Nalo kupitia mimi, Bwana, ili wengine waweze kuona. Jalia Hilo likolee chumvi na kitu halisi, kusudi wengine waweze kuona.” Naam, bwana.

²¹³ Sasa, kama Yeye ni Yakini yetu, hapawezi kuwapo na yakini nyingine. Huwezi kuwa na, tuseme, “Vema, ka—kanisa langu ndilo yakini yangu. Kanuni yangu ya imani ndiyo yakini yangu.” Ikiwa Kristo ndiye Yakini yako, unaliadini Neno la Kristo. Hakuna njia nyingine ya kufanya hilo.

²¹⁴ Mnajua, ninafikiri juu ya wakati ambapo Yeye aliniokoa. Nitawaambia ni kwa nini ninasimama jinsi ninavyosimama; sio niwe tofauti. Nilijielezea vizuri juu ya hilo; ninatumaini mimejieleza. Lakini mimi. . . Wakati Kristo aliponiokoa, kulikuwako na mamiloni ya watu wakipapasapasa katika dhambi. Wakati aliponiokoa, Yeye alikuwa na kusudi katika kufanya hivyo. Alikuwa na kusudi katika kuniokoa. Yeye aliona tu mjinga kama mimi, na—na, kwa njia moja ama nyingine, wakati kulikuwako na watu wengi sana werevu, watu wenye uweza zaidi, watu ambao wangaliweza kulifanya. Mimi hapa, bila hata elimu ya darasa la saba, wakati kulikuwako na watu waliosoma shuleni na wakapata madigrii, na madaktari wa—wa uungu na falsafa, na kadhalika. Lakini wakati Kristo aliponiokoa, Yeye alikuwa na kusudi katika kufanya hilo, la siyvyo asingeniokoa.

²¹⁵ Sikilizeni, ndugu. Ninawapenda, nanyi mnajua hilo. Lakini nimedhamiria moyoni mwangu ya kwamba kamwe sitaliacha Neno hilo. Nitakaa pale pale. Hilo ndilo Yakini yangu, niliyofungiwa, miaka hii yote. Sasa, Yeye alikuwa na kusudi katika kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Nami ninakusudia kulitimiza kusudi hilo, kukaa pamoja na Neno hilo; sio kuwa tofauti, sio kuwa mchoyo, bali kuwa mwaminifu na mkweli kwa Mungu. Hiyo ni kweli.

²¹⁶ Sasa, mwajua, kifo cha Kristo kilikuwa na yakini kwake. Kila mtu aliogopa kifo, hata yule nabii mashuhuri Ayubu. Watu

wengi waliogopa kifo, woga. Nao watu daima walikiogopa. Lakini wakati Kristo alipokuja na kujitwika kifo, Yeye alifanyika Yakini kwa wale walioogopa kifo. Katika Waebrania 2:14-15, “Yeye alijitwika mfano wa mwanadamu,” apate kufa kama mwanadamu, kuilipia adhabu. Lakini, kwenye Pasaka, Yeye alitokea na funguo za mauti na kuzimu. Yeye alikuwa ameyashinda. Akaja, akasema, “Msiogope. Mimi Ndimi nalikuwa nimekufa, na ni hai hata milele.”

²¹⁷ Nayo Yakini yetu iko juu Yake, hiyo ni kweli, katika Yeye. Naye alikuwa ni Neno kamilifu la Mungu. Alikuwa mkamilifu sana hata, wakati aliponena Neno Lake, liliumba. Liliukomesha upepo. Li—lilifanya biskuti, na samaki waliopikwa, kwa Neno Lake tu. Mnaona? Hapakuwapo na kizuizi. Yeye alikuwa ni mkamilifu sana. Alisema Yeye na Neno walikuwa ni Mmoja.

²¹⁸ Yeye alikuwa ni upendo wa Mungu, katika Yohana 3:16. Aliufanya mwili, usiozaliwa kwa kujuana kimwili, chini ya kule kuanguka. Lakini alizaliwa kwa nguvu umbaji za Mungu, hata Mungu Mwenyewe aliishi katika mwili huu na kulionyesha wazi Neno Lake. “Naye Mungu alikuwa katika Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake,” akifanya yakini kwa ajili ya mwaminio yeyote. Naye akaenda kaburini Mwake, amejitwika mzigo wa dhambi, akalipia adhabu yake. Kisha akafufuka kwenye asubuhi ya Pasaka, akiwa na funguo za mauti na kuzimu. Ni yakini kwa mtu yeyote anayeogopa mauti.

²¹⁹ Hebu niseme hili. Sijui ni Jumbe ngapi zaidi itanibidi kuhubiri kabla sijaondoka. Lakini kama wewe ni mwaminio halisi katika Mungu, na umezaliwa mara ya pili, usiogope mauti. Ndilo jambo zuri kuliko yote lingaliweza kukutokea, karibu hivyo. Paulo alisema, “Kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida.” Hakika. Ni... Kamwe usiogope mauti. Wathesalonike wa Pili, “Tunanyakuliwa pamoja na wapendwa wetu, kukutana na Yeye hewani.” Ni ahadi ya jinsi gani! Hiyo ni yakini ya jinsi gani, kumwamini Kristo, kuufanya moyo wangu useme “amina” kwa kila Neno katika Kitabu Chake!

²²⁰ Kile asemacho, ninakiamini, pia. Hilo ninajua, ya kwamba Roho Mtakatifu ndiye Dira yangu, kwa sababu huniongoza kwenye Yakini Yake, mnaona, Nyota Yake ya Kaskazini; Kwake, Nyota ya Kaskazini. Yeye ni Yakini yangu, Jua langu, Nguzo yangu, Nyota yangu ya Kaskazini. Loo, jamani!

²²¹ Yeye ni tofauti sana na wengine niwaonao, daima kuna kitu kinachovuta, kamba fulani unayopaswa kuvuta. Lakini, katika Hili hapa, huvuti chochote. Jambo pekee, linashushwa kwako. Ndilo Yakini. Kristo ndiye Yakini yetu.

²²² Angalieni jinsi Neno Lake lilivyo tofauti. Hilo Neno limekuwako tangu zamani. Agano Jipya na la Kale zinaafikiana, kama kipande cha ubao kilichoumana kikishikana pamoja. Hakuna kitu kilicho nje ya utaratibu. Watu wengi walikiandika

Kitabu hicho, vitabu hivyo sitini na sita vya Biblia. Waliandika wakiachana kwa muda wa mamia na mamia ya miaka, mmoja hamjui mwenzake. Basi ni jambo gani lililotukia? Huwezi kulifanya Neno moja lipinge lingine. Kweli. Hiyo ndiyo sababu.

²²³ Nimewasikia watu wakisema, “Biblia inajipinga Yenyewe.” Nitahubiri kote katika Marekani hii kwa mwaka mmoja, moja kwa moja, na kuwaacha wahudumu wachukue sadaka na niwape kila kitu, kama utanionyesha ambapo Neno la Mungu linajipinga Lenyewe. Kweli. Nimetoa ahadi hiyo kwa miaka mingi. Hakuna mtu ambaye ameichukua bado. La. Kwa sababu, Hilo halijipingi. Ni maskini akili yako finyu, ambapo una—unajaribu kulifanya Hilo liseme jambo fulani ambalo halisemi. Kweli. La. Neno la Mungu halijipingi Lenyewe. Yeye ni, ni . . .

²²⁴ Sasa, madhehebu yatapingana. Hayo ni kama nyota hizi zingine, mnaona. Yatalea kote, kila wakati, kama dunia. Yanageuka katika dunia, na kuuzunguka ulimwengu. Nayo dunia inazunguka na kuwapiga wote pigo la kishindo.

²²⁵ Lakini kamwe haiondoki kwenye Nyota ya Kaskazini ya Mungu, Neno Lake, ambako dira huelekeza Kwake. Daima ni vile vile, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Huyo ndiye Yakini. Hapo ndipo mahali.

²²⁶ Unaweza kuangalia *hili* hapa. Leo hii liko hapa, na kesho linaamini jambo lingine. Kesho yake, liko, mahali pengine. Ndivyo hivyo. Halina msimamo, ndani na nje, nje na nje, na ndani na ndani, na kadhalika.

²²⁷ Lakini, wewe uweke moyo wako moja kwa moja kwenye Neno la Mungu. “Na mbingu na nchi zitapita, bali Hilo halitapita kamwe.” Hilo ndilo Yakini. Huo ndio Msingi imara. Hiyo ndiyo—hiyo ndiyo Dira yangu, Tanga langu. Hilo ndilo Kiongozi wangu. Hilo ndilo Taa yangu, ni juu ya Yakini hiyo ya Neno la Mungu. Nimefungiwa pale, Milele, pamoja na Yeye. Amina. Wengine wanaweza kufanya watakayo; hiyo ni juu yao. Lakini, kwangu mimi, ni Yakini hii. Ninalitaka hilo kama Yakini yangu. Huenda wakahama na kugeuka, na kadhalika, bali si Neno Lake. Daima litabaki vile vile. Yeye daima hubaki mkweli kwa Neno Lake. Sasa mfanye Yeye Yakini yako.

²²⁸ Katika nyakati za matatizo yangu huko nyuma, wakati nilipoipoteza familia yangu, nao uhai wangu nusura uondolewe kwangu. Msichana wangu mdogo alikufa, huku nikimwombea, na baada ya mimi kuwa mitaani, mchana na usiku, nikihubiri na kuomba, na kujaribu kufanya yaliyo haki. Mmeisikia hadithi ya maisha yangu. Wengi wenu mliisoma. Na, jamani, ilifikia mahali, hata ni—nikamwona mke wangu akifa, papo . . . nami nikiushika mkono wake. Mimi . . . Mtoto wangu mchanga akawa mgonjwa, saa chache baada ya hapo. Nami nikashuka pale na kuomba, kwa yote yaliyokuwa ndani yangu. Ilionekana kama shuka jeusi lilishushwa chini, akakataa kujibu maombi yangu.

229 Ndipo Shetani akanijia na kusema, “Unaona, wewe una umri wa kama miaka ishirini tu. Na hapa, wewe, yale yote uliyofanya! Na, wewe, umejiachilia vibaya. Na umefanya mambo haya yote. U—umeacha ujana wako wote, karibu umeupoteza, wakati ulipaswa kuwa huko nje ukiwa na wakati mzuri sana kama hao vijana wengine. Nawe hapa ulisimama pembeni mwa mtaa, ukilia na kuomba. Ulienda usiku kucha kwa zamu, hospitalini, saa baada ya saa. Na inapofikia kwa damu yako mwenyewe na mwili, Yeye anakataa kukusikia.” Huo ulikuwa ndio wakati mmoja niliojaribiwa.

230 Lakini ilitokea nilikumbuka nyuma. “Ninayo Yakini. Ingawa ataniua, bado nitamtumaini. Sijali kijacho wala kiendacho.”

231 Seneta wa jimbo la Indiana, Sam Isler, alikuja, pia. Amekuja maskanini. Yeye ni marehemu sasa, yapata miaka miwili. Mtu mwema. Naye alikuwa akininii...Alikuwa akishuka barabarani.

232 Nilikuwa nikipanda juu, kuomba, juu kaburini ambako mke wangu na mtoto mchanga walikuwa wamelala. Ilikuwa ni mara baada ya mafuriko ya '37. Nilikuwa nimevaa jozi ya buti, nami nilikuwa nikipanda barabarani, nikilia.

233 Maskini Billy, mwanangu, alikuwa karibu kufa, pia. Nao madaktari walikuwa tayari wamesema karibu hapakuwapo na lolote zaidi wangelimfanyia. Na—naye alikuwa na namna fulani ya ugonjwa wa kuhara damu ambao wasingeweza kuukomesha, maambukizi.

234 Basi nilikuwa nikilia, nikiomba, ndipo nikawaza. Vema, nilikuwa ningali ninamshikilia Mungu. Nilikuwa nikipanda barabarani, nikilia.

235 Nikawazia ningepanda juu na kusikiliza. Nilikuwa nikiketi pale, mnamo jioni, karibu na kaburi. Ningemsikia maskini hua akishuka pale na kuanza kuimba. Ninasikia misonobari ikipulizia, na u—u—upepo kupitia kwenye—upepo kupitia kwenye misonobari, hasa. Nayo ilisikika kana kwamba ingesema:

Kuna Nchi iliyo ng'ambo ya mto,
Wanaiita tamu milele,
Tunaufikia tu Ufuko huu kwa shahada ya imani;
Mmoja baada ya mwingine twaingia langoni,
Pale tukaishi pamoja na wasiopatikana na mauti,
Siku moja watapiga hizo kengele za dhahabu kwa ajili yangu na yako.

236 Ningesimama hapo, nilie, na kuangalia juu. Nami ningemwambia mke wangu na mtoto, niseme, “Na—najua ya kwamba hamko hapa. Hapa ni mahali tu ambapo nilipandikiza

mabaki niliyoyashika kwa mikono yangu. Lakini mahali fulani, ng'ambo ya mto, mko huko."

²³⁷ Kwa hiyo, lakini, mnaona, ni—nilikuwa nikikwea kwenda mahali pale, siku moja, kuketi kwenye kaburi. Nilikuwa na jozi ya buti, nikitembea. Motokaa kuukuu ikaja nyuma yangu, ikasimama. Ilikuwa ni Bw. Isler, seneta wa jimbo. Akaruka akatoka kwenye motokaa. Akaiegesha halafu akarudi. Akanikumbatia kwa mikono yake, kasema, "Billy, hakika ninakuhurumia."

Nikasema, "Hilo ni sawa, Ndugu Isler."

²³⁸ Naye akasema, "A—afadhali nisingalisimama." Aliona nilikuwa nikilia.

Nikasema, "Hilo ni sawa, Bw. Isler."

Naye akasema, "Nitakuuliza jambo fulani, mwanangu."

Nikasema, "Vema. Endelea uniulize."

²³⁹ Akasema, "Nimekuona ukisimama pale mimbarani hata nikafikiri ungekufa." Kasema, "Nimekuona ukifunga mpaka ungekuwa dhaifu sana ningekuhurumia, na," kasema, "kuingia na kutoka, na kuingia na kutoka, mchana na usiku." Akasema, "Halafu mke wako na mtoto mchanga mle ndani, unaona, unayaangalia mambo hayo." Akasema, "Kristo anamaanisha nini kwako sasa?"

Nikasema:

Wewe ndiwe Kijito cha faraja yangu yote,
Zaidi ya uhai kwangu,
Ni nani niliye naye duniani mbali na Wewe?
Ama ni nani Mbinguni ila Wewe?

²⁴⁰ Mnaona, nilikuwa nimeipata hiyo Yakini, kile Kitu fulani ambacho kilinishikilia wakati dhoruba zikivuma.

²⁴¹ Mtu fulani aliniambia, kasema, "Billy, hivi ulihifadhi dini yako wakati wa matatizo yako?"

Nikasema, "La. Ilinihifadhi." Mnaona?

²⁴² Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Nilikuwa nimefungiwa Kwake wakati nguvu zangu zilikuwa zimekwisha, na hakuna jambo ningaliweza kufanya. Nanga yangu ilishikilia ndani ya pazia la Neno Lake huko ng'ambo.

²⁴³ Ambako, wakati mwingine siliielewi. Wakati mwingine nawazia, "Ni kitu gani kinachonifanya kufanya mambo nifanyayo?" Kuna Kitu fulani kilicho ndani yangu, kinachonidundadunda. Siwezi kujizuia kufanya hivyo, ndugu.

²⁴⁴ Nilikuja Phoenix, hivi majuzi, nikiwa nimedhamiria nisingeshambulia dhehebu lolote tena. Muda si muda mwajua, ono likatokea mbele zangu, usiku wa kwanza, nami nikajiona nikielekea jangwani. Kitu fulani kikanigeuza, kikanionyesha kanisa kubwa mno, la kale, baridi, kasema, "Kaa *mle*, kabla

hujaenda *kule*.” Loo, jamani! Kuna kitu fulani nisichoweza kujizuia kufanya. Ni yakini iliyo ndani yangu. Ni zaidi ya uhai wangu, kwangu mimi. Naam. Siwezi kukibadilisha kadiri nisivyoweza kuibadilisha rangi ya macho yangu. Nisingeweza kufanya hivyo.

²⁴⁵ Sasa, kwa neema Yake, nimefungamanishwa Kwake, Yule ambaye alisema, kama alivyofanya katika siku za Musa, “MIMI NIKO.”

²⁴⁶ Musa, mwajua, alikuwa na yakini. Wakati alipokuwa kule chini, alikuwa na theolojia yote mwanadamu angaliweza kuwa nayo. Naye akajaribu sana. Alikuwa ni mwanajeshi. Aliangalia nje ya madirisha. Na kwa imani . . . Sikilizeni. Sasa, kumbukeni. “Kwa imani, Musa alihesabu shutuma la—la Kristo kuwa ni utajiri mkubwa kuliko hazina za Misri.” Alikuwa na imani na yale aliyokuwa akifanya. Aliyaamini kabisa. Alijua ya kwamba alikuwa amelelewa kwa kusudi hilo. Lakini alishindwa. Aliondoka akaenda kuwachunga kondoo. Naye akashindwa.

²⁴⁷ Lakini siku moja, huko nyuma upande wa nyuma ya jangwa, alikutana na Yakini. Alifikia mahali ambapo alikutana na Kitu kilichokuwa halisi. Kulikuwa na kichaka kilichowaka Moto. Hakutaka kuchukua majani hayo na kuyapeleka kwenye maabara, aone sababu ya hayo kutoteketea. Aliketi tu karibu Nayo. “Vua viatu vyako, Musa.”

²⁴⁸ “Nitashuka niende nikamuulize mchungaji wangu, ‘Vipi kuhusu Hili?’” Hakuwa na wakati wa kufanya hivyo.

²⁴⁹ Hana budi kuvua viatu vyake. Basi wakati aliposikia Mle ndani, kulikuwako na Neno la Mungu aliye hai, lililokuwa kwenye kichaka hicho. “MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Ninakumbuka ahadi Yangu niliyofanya na Ibrahimu. Ninakumbuka agano Langu, nami nimeshuka kuwakomboa.”

²⁵⁰ Sasa, basi, yeye alikuwa na Yakini. Alikuwa amefungwa kwenye hiyo mradi tu alikuwa hai, nayo ikampeleka Mbinguni. Yeye alikuwa amefungwa kwenye Yakini hiyo, haijalishi kile yeyote wa wanatheolojia alichosema. Hakuhitaji mtu yeyote kumwelezea Hiyo. Alijua Hiyo. Alikuwa amekutana na Mungu, nayo ile Sauti, ile Nguzo kubwa ya Moto iliyomwongoza kupitia nyikani, hata kwenye nchi ya ahadi. Hiyo Nguzo ya Moto mle ndani, ilikuwa na Sauti ndani Yake, nayo Sauti hiyo ilikuwa ni Sauti ya Mungu iliyolithibitisha Neno. Amina.

Natumaini hamlali sasa. Angalieni.

²⁵¹ Hiyo Nguzo ya Moto ilinena Neno, na kulithibitisha, kulifanya lioneshe ameyanukuu Maandiko. “Mimi ndiye Mungu aliyefanya ahadi kwa Ibrahimu. Mimi Ndimi. Hiyo ndiyo shida ya Israeli. Hiyo ndiyo shida kule chini. Ninaikumbuka ahadi Yangu, nami nimeshuka kuona kwamba imetimizwa.”

²⁵² Mungu humtumia tu mwanadamu, kutenda kazi naye. Hatumii madhehebu. Hatumii mitambo. Angaliweza kufanya hivyo. Lakini, Yeye alimchagua mwanadamu. Hiyo ni kweli. Angeweza kuchagua nyota, upepo, ama chochote, kuhubiri Injili. Lakini, Yeye alimchagua mwanadamu. Yeye hajibadilishi Mwenyewe. Siku zote ni yeye yule.

²⁵³ Alichagua Damu kwa ajili ya wokovu. Elimu wala chochote kingine kamwe hakitachukua mahali Pake. Damu ndiyo njia ya Mungu ifaayo kwa ajili ya wokovu. Hiyo ni kweli.

Basi sasa, ninawatakeni muone, Yeye hawezi kubadilika.

²⁵⁴ Wakati aliponena na Musa, Yeye alisema, “Musa, ninakutuma huko chini. Lakini, kabla hujaenda, ninataka kukuthibitisha ya kwamba Mimi ni Mungu.” Kasema, “Una nini mkononi mwako hapo?”

Kasema, “Fimbo.”

²⁵⁵ Kasema, “Itupe chini.” Nayo ikageuka ikawa nyoka. Akaichukua tena. Ikarudi tena, fimbo.

²⁵⁶ Loo, wakati Musa alipofika mahali ambapo waigaji waliinuka, wakijaribu kuiga! Wakati alipoitupa fimbo yake chini, na kusema, “Hapa, Farao, nitakuonyesha yale Mungu aliyoniambia nifanye. Nitaitupa fimbo hii chini, uitazame ikigeuka kuwa nyoka.” Ikageuka.

²⁵⁷ Farao akasema, “Ninao hao jamaa, pia. Dhebebu langu linaweza kufanya hivyo.” Kwa hiyo, wakaja na kuwachukua waigaji fulani.

²⁵⁸ Musa alifanya nini? Yeye alisimama papo hapo. Kwa nini? Alikuwa amekutana na Mungu. Alijua huyo alikuwa ni Mungu. Alikuwa ametimiza sehemu yake. Ni wakati wa Mungu wa kutenda kazi basi. Akakaa pale pale.

²⁵⁹ Biblia ilisema jambo lilo hilo litajirudia katika siku za mwisho, “Kwa kuwa kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa.” Ni kweli. Mnaona?

²⁶⁰ Lakini alisimama pale. Ndipo akauona mkono wa Mungu ukishuka, naye nyoka huyo akawameza kwa haraka hao wengine. Hivi mlipata kuona mwisho wa hizo fimbo? Zilikuwa katika tumbo la fimbo hii moja. Musa aliwaongoza wana wa Israeli kupitia nyikani, akiwa na fimbo iyo hiyo, pamoja na hao nyoka wote ndani yake, nadhani.

²⁶¹ Kwa nini? Mnajua ni kwa nini? Wakati Musa alipokutana na kichaka hiki kilichowaka moto, mwajua, nacho kichaka hicho kilichowaka moto kikadai, kikathibitisha kwamba ni Mungu. Nuru hiyo, Nguzo hiyo ya Moto, iliyothibitisha kwamba ni Mungu. Nami naamini ya kwamba Mungu alikuja ndani ya Musa, kwa sababu, mwangalie katika nguvu zake za uumbaji. Musa basi aling’aa kwa huo Moto.

262 Mnajua mahali ninakoelekea sasa, sivyo? Hakika, kama Pentekoste.

263 Angalia, Musa alikuwa na Moto. Huo Moto ulikuwa ndani ya Musa. Kwa sababu, lolote alilosema Musa, haikuwa ni Musa. Ilikuwa ni Mungu akinena. Naye akafanya ishara yake, kwa sababu Nguzo ya Moto iliondoka kichakani ikaja juu ya Musa. Amina.

264 Loo, ndugu, mnaona ninalomaanisha? Yesu yeye yule aliyepaa juu, alirudi tena kwenye Siku ya Pentekoste, katika mfano wa Roho Mtakatifu na Moto. Anapaswa kuwa juu ya watu, akifanya jambo lile lile alilofanya, maana Yeye alisema angefanya hivyo. Tuko wapi? Mnaona ninalomaanisha? Musa, ule Moto ulikuwa ndani ya Musa. Uliondoka kichakani, ukaja juu ya Musa.

265 Sisi hujaribu kuweka Moto kwenye tanuru. Hilo karibu ndilo lote tulilo nalo. Tunachohitaji ni Moto wa Roho Mtakatifu, Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza Israeli. Hakika.

266 Loo, mnasema, "Sasa, Ndugu Branham, ningekuwa mwangalifu kuhusu hilo."

267 Sasa, ngoja kidogo. Wakati Paulo, yule mwanathelopia mashuhuri aliyekuwa na ujuzi mwingi sana, bali njiani akienda Dameski, ndipo aliangukwa chini. Aliangalia juu na palikuwapo na ile Nguzo ya Moto. Alijua hiyo ilikuwa ni Mungu. Alikuwa ameiona Hiyo ikithibitishwa katika Biblia, ilikuwa ni Mungu. Naye akamwita, "Bwana." Kasema, "Bwana, U nani Wewe? Nifanye nini?"

Akasema, "Mimi ni Yesu."

268 Hilo lilitosha. Paulo alikuwa na Yakini. Alijua ya kwamba Mungu wa Agano la Kale alikuwa ni Yesu Kristo wa lile Jipya. Hapo alitiwa nanga, na hukuna kitu kinachopaswa kumtikisa. Hakika. Alikuwa na thibitisho. Kwa nini? Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza watu Wake kutoka Misri kuingia Israeli, kuingia Palestina, Nguzo hiyo hiyo ya Moto ilikuwa imesimama pale ikidai kwamba ni Yesu Kristo. Ndipo akajua mahali alipokuwa. Ndipo akawa tayari. Mara alipoponywa na kujazwa na Roho Mtakatifu, alikuwa tayari kuenda. Mnaona?

269 Lakini, yeye alikuwa na Yakini. Ilikaa pamoja naye, mbele ya Agripa na wanaume wote mashuhuri wa siku hizo, na wanawake. Alisimama hapo akilitetea Neno. Kwa nini? Alijua ya kwamba Neno lilikuwa ni Mungu.

270 Ni nani aliyekiandika kitabu cha Waebrania? Paulo, hakika. Alivuviwa kufanya hivyo. Lakini ni kwa nini? Nguzo hiyo ya Moto iliyokutana naye ilikuwa ndani yake. Hiyo ndiyo sababu angeweza kuandika.

271 Hiyo ndiyo sababu Musa aliandika vitabu vya kwanza vinne vya Biblia, kwa sababu, Nguzo hiyo ya Moto. Yeye angejuaje

kamwe jinsi uumbaji ulivyoanza? Angewezeje kamwe kujua juu ya mengine? Kwa sababu, Nguzo ile ile ya Moto iliyokuwa ndani yake, iliyokuwa kwenye kile kichaka, iliondoka kichakani na ilikuwa juu yake. Nayo ilihakikishwa na kuthibitishwa kwamba ilikuwako. Kora na hao wengine wanataka kuanzisha dhehebu dhidi Yake, bali halikufanikiwa. Lilishindwa. Musa alikuwa na hiyo Yakini.

²⁷² Paulo alikuwa na Yakini iyo hiyo, Nguzo ile ile ya Moto, Roho Mtakatifu yule yule, Mungu yeye yule, sio “Nilikuwa,” ama “Nitakuwa,” Yule “MIMI NIKO,” a-ha, wakati uliopo, daima.

²⁷³ Yoshua alikuwa na Yakini. Hiyo ni wakati alipokutana na Jemadari Mkuu, Jemadari Mkuu wa jeshi la Israeli. Naye akamwambia “zizunguke kuta.” Wote walikuwa wamejiimarisha ndani. Loo, jamani, mnanena kuhusu, ni vigumu kuingia? Ni vigumu kufanya uamsho mle, kwa kuwa hakuna mtu angemruhusu kuingia. Wote walikuwa wamemzingira, yeye. Lakini alikutana na Jemadari Mkuu. Alimwambia la kufanya. “Jivike tu silaha zote za Mungu, na uendelee kutembea taratibu.” Amina. “Hizo kuta zitaanguka.” Ndipo wakati watu walipopaza sauti, na parapanda zikalia, hiyo ilikuwa ndiyo yakini yake. Aliingia moja kwa moja kwa uamsho wake basi, akaingia moja—moja kwa moja Yeriko. Hakika. Yeye alikuwa na Yakini, Neno la, kutoka kwa Jemadari Mkuu.

²⁷⁴ Yohana, wakati alipokuwa kijana mwanamume, basi alijua ilimbidi kufundishwa. Alikuwa anaenda—alikuwa anaenda kulazimika kumtambulisha Masihi. Alikuwa ndiye. Kamwe hakujua Yeye alikuwa ni Nani. Alikuwa mahali fulani. Basi Yohana alijua ya kwamba asingechukua tu ujuzi wa seminari. Ilimbidi kuwa na Yakini. Ilimbidi kuwa na kitu fulani kuwa ni kweli kabisa.

²⁷⁵ Sasa, ndugu zangu, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Wahudumu, sio kuwa tofauti, sio kuwa katili, bali kuwa mwaminifu, hivi hamuwazii hii ndiyo siku, katika machafuko haya yote tunayoishi ndani yake, inatubidi kuwa—inatubidi kuwa na hakika kuhusu jambo hili? Kuna tofauti nyingi kupita kiasi.

²⁷⁶ Naye Yohana alijua ilimbidi kuwa na hakika kabisa, kwa hiyo kamwe hakwenda kwenye shule ya baba yake. Hapo hakuna kitu kilichosemwa ya kwamba alirudi kujifunza kuwa kuhani. Bali alienda nyikani, naye alikuwa nyikani mpaka wakati wa kuitwa kwake.

²⁷⁷ Ndipo akaja karibu, nao umati ulikuwa umesimama pale. Alikuwa na hakika sana ya kwamba Masihi alikuwa katika siku yake, kwa sababu yeye alikuwa ndiye aliyechaguliwa kumtambulisha Masihi huyu, kwa sababu Malaki 3 ilisema hivyo. “Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu. Naye atayatengenza mapito.”

278 Yohana alijua mahali alipokuwa amesimama. Haijalishi ni makuhani wangapi wangesema, “Unamaanisha kusema wakati, tulio nao hapa, dhabihu ya kila siku itaondolewa?”

279 Yeye akasema, “Utakuja wakati ambapo Mwana-kondoo wa Mungu atakuja, ambaye ataiondolea mbali hiyo dhabihu.” Akisimama katika matope, masharubu juu ya uso wake, hata ungemfukuza nyumbani mwako leo hii. Kulikuwako... Mnaona?

280 Mungu hayuko katika tabaka na madoido, kama tunvyojaribu kumwingiza ndani, na sisi Wapentekoste. Mungu yuko katika unyenyekevu.

281 Huyu hapo, amesimama. Mtazameni. Naye alikuwa akitambulisha. Yeye, yeye alisema... Alikuwa na hakika sana kwamba Yeye alikuwa pale, akasema, “Yupo Mtu anayesimama katikati yenu, Ambaye hata hamumjui.” Loo, jamani! Ni kemeo la jinsi gani! “Yupo Mtu anayesimama miongoni mwenu, sasa hivi, msiyemjua.”

282 Nashangaa kama lingesikika la kukufuru kama ningalimwiga kwa dakika moja. Labda afadhali nisimwige. Mtu miongoni mwenu, msiyemjua. Mnadai kwamba mnamjua, bali hamumjui. Golgotha, wanamwua Mungu yeye yule wanayedai walikuwa wakimtumikia. Hawakumjua.

Yohana alisema, “Yupo Mtu miongoni mwenu, nanyi hamumjui.”

283 Basi siku moja aliangalia huko nje, naye kabisa alimwona Hua akishuka kutoka Mbinguni, na Sauti. Hakuna mtu mwingine aliyemwona. Hakuna mtu mwingine aliyeisikia. Lakini yeye alimwona, na Yeye alikuwa ni yakini; sio Profesa Jones, wala mtu mwingine. Ilikuwa, “Yeye Ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, Huyu Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.” Hilo ni thibitisho la Kiungu la Mungu akilitimiza. Ilikuwa ni yakini. Hapakuwapo na—na swali niani mwa Yohana. Hiyo hapo, vile tu Mungu alivyosema ingetukia. Ilikuwa ndiyo hiyo hapo. Kwa hiyo, huyo Hua juu ya Mtu wa kawaida alikuwa—alikuwa ndiye yakini ya Yohana. Alijua ilikuwa ni kweli.

284 Sasa nitafunga kwa kusema maneno haya machache. Hivi hamfikiri tunahitaji Yakini? Hamfikiri tunahitaji kitu kilicho halisi? Hakika. Tunahitaji kitu fulani, hicho kitu fulani ambacho unaweza kusema, “*Hiki Ndicho*,” uweke mikono yako juu yake. “*Hiki Ndicho*,” tunaweza kuona. Tutafanyaje hilo? Kila mtu anasema, “*Hiki Ndicho. Hiki Ndicho.*” Lakini hiyo haina budi kuwa ni ya Kimaandiko, yakini.

285 Hebu niwape tu jambo dogo la kibinafsi kabla sijafunga. Ndugu, dada, nilipofanya chaguo langu, kama nilitaka kubaki pamoja na kanisa la Kibaptisti, ama nini. Ni zuri tu kama lolote—lolote la hayo, kwangu mimi, kundi tu la watu

waliowekwa pamoja, ambalo ni sawa. Lakini ilipofikia wakati ambapo iliwabidi kuniambia ya kwamba ilinibidi kufanya mapatano juu ya Neno, sasa, hilo, mimi sijaumbwa kwa hicho. La. Mnaona? Neno ndilo la kwanza. Mnaona?

²⁸⁶ “Vema,” wakasema, “usipofanya *hivyo*, huwezi kuendelea kuwa wa kanisa la Kibaptisti.”

²⁸⁷ Nikasema, “Sifanyi. Sikuokolewa na kanisa la Kibaptisti. Ilikuwa ni Yesu Kristo, mnaona, aliyeiniokoa.”

²⁸⁸ Yeye ndiye Mkataa wangu. Ndiye Msimamo wangu. Ndiye Yakini yangu. Ndiye Nguzo yangu ya kujifungia. Hapo nasimama.

²⁸⁹ Sasa, kama nina kitu kibaya, basi Mungu kamwe hatakihibitisha. Lakini kama una kitu cha kweli, Mungu anawajibika kukithibitisha. Haya basi. Na hilo ndilo thibitisho lake. Mnaona? Kama ni kweli, Mungu anawajibika kuthibitisha kwamba ni kweli. Kama ni uongo, hatakuwa na uhusiano wowote nao.

²⁹⁰ Kwa hiyo, nakumbuka, baada ya uamsho wangu wa kwanza. Nilikuwa huko chini mtoni, nikibatiza. Nikamchukua mtu wa kumi na saba. Mke wangu, msichana mdogo akisimama ufukoni wakati huo. (Sikuwa nimemwoa mke wangu wa kwanza aliyefariki.) Naye huyo hapo, ufukoni. Nao wote walikuwa wamesimama pale, mamia na mamia ya watu, naam, elfu nne ama tano, labda wengi zaidi, juu chini ufukoni mwa mto, alasiri yenye joto kwelikweli katika Juni.

²⁹¹ Nikaingia huko majini, nami nikamchukua mtarajiwa, yapata mtu wa kumi na saba, kumbatiza. Nilikuwa na karibu mia tano, baada ya uamsho wangu, wa kubatizwa. Basi nikaingia majini pamoja na mtu huyu. Nikaanza kuinua mkono wangu. Nikasema, “Baba wa Mbinguni, wakati mimi . . .”

²⁹² Basi yapata wakati huo, Kitu fulani kikanitikisa. Nikawaza, “Kiko wapi?” Nikaangalia kote. Kila mtu alikuwa ameinamisha vichwa vyao, loo, kadiri nilivyoweza kuona. Huko juu kabisa ufukoni, kulikuwako, loo, magari na watu wamelundikana kote kwenye kuta, na kadhalika. Nikaangalia tena. Nikasikia Sauti ikisema, “Angalia juu.” Nami niliogopa kuangalia juu. Nilikuwa ni mtoto tu. Tunayo picha Yake.

Nikasema, “Baba . . .”

Kitu fulani kikasema, “Angalia juu.”

²⁹³ Nikaweka mkono wangu chini. Jamaa huyu mdogo, niliyekuwa nimbatize, akaniangalia usoni. Akasema, “Vema, Ndugu Bill?”

Nikasema, “Ulisikia Hiyo?”

Akasema, “La.”

Nikasema, “Baba wa Mbinguni . . .”

Akasema, “Angalia juu.”

²⁹⁴ Nikaangalia juu, namna *hii*. Ndipo kutoka angani ikashuka Nguzo ya Nuru ikizungukazunguka, Sauti ikitoka Kwake, ikinguruma, ikishuka. Kasema, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kukutangulia kuja kwa Yesu Kristo mara ya kwanza, vivyo hivyo wewe umetumwa.” Ee Mungu! Nikaangalia Nuru hiyo. Nilikuwa nimeiona, tangu mvulana mdogo.

Nikajaribu kuwaambia watu. Wakasema, “Umerukwa na akili.”

²⁹⁵ Lakini utafiti wa sayansi, hayati George J. Lacy, wakati alipoichunguza, wakati walipoipiga picha Yake, Hiyo hapo, vile vile hasa. Iliyonesha katika hiyo picha. Thibitisho la sayansi inathibitisha kwamba Hiyo ni sahihi. Kwangu mimi, haijawahi kuniambia jambo moja ila linaloambatana na Maandiko haya kikamilifu.

²⁹⁶ Wakati, nilipouona huo Moto na kuusikia, na kumwona kila mtu akipiga mayowe, wakizimia, na kuanguka, wakiangalia pale, na kuelekeza kwenye Nuru hiyo. Gazeti, gazeti la Louisville, liliyaandika makala hayo mashuhuri. Yakaenda kwenye Associated Press, kote kupitia Canada, kila mahali, “Nuru isiyo ya kawaida imetokea juu ya mhudumu wa mtaani wa Kibaptisti wakati akibatiza.” *Isiyo ya kawaida*, “ngumu kueleweka.” Ni mara ngapi wameipiga Hiyo picha? Karibu kila mtu hapa ndani, nadhani, anayo nyumbani mwenu. Iko kule Washington, DC, ina hakinakili kama “Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha, kupigwa picha kisayansi.”

²⁹⁷ Ilikuwa ni kitu gani? Nuru ile ile, Sauti ile ile, ilinena na kusema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ni Sauti ile ile. Kwangu mimi, ni Nguzo ile ile ya Moto iliyokuwa huko nyuma, kwa sababu inafanya kazi zile zile. Yesu alisema, “Nimetoka kwa Mungu na ninaenda kwa Mungu. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena.” Yeye alikuja. Akasema, wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, kwenye ile karamu, alisema, “MIMI NIKO AMBAYE NIKO.” Mnasema . . .

²⁹⁸ “Vema, Wewe hujapata umri wa zaidi ya miaka hamsini, lakini, Wewe ulisema, unasema Wewe ‘ulimwona Ibrahimu’?”

Akasema, “Kabla Ibrahimu hajakuweko MIMI NIKO.”

²⁹⁹ Huyo hapo. Ilikuwa ni kitu gani? Hiyo Nuru, huo Moto, huyo Mungu, huyo Roho. Mungu ni Moto uwakao. Yeye ni Nuru. Na Hiyo hapo, katika, imedhihirishwa katika Yesu Kristo. Iirudi wakati Yesu alipofufuka kutoka kaburini.

³⁰⁰ Lakini kwenye siku aliyokutana na Paulo, akishuka kwenda Dameski, alikuwa amerudi kwa Mungu tena, kwa kuwa Yeye alisema, “Mimi ni Yesu, Ambaye unamwudhi.”

301 Ndugu, msilale. Hivi hamwoni ya kwamba Mungu yule yule yuko miongoni mwetu sasa hivi, akijithibitisha Mwenyewe, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Huyo ndiye Yakini yangu.

302 Hajawahi kuniambia jambo moja...Kama aliniambia jambo moja ambalo lilikuwa ni kinyume na Maandiko haya...

303 Sijawahi kuwa na mtu yeyote kusimama mbele yangu bado na kulikanusha. Jamaa mmoja alisema atalikanusha, wakati mmoja, wala hakulikanusha. Hakujitokeza. Alikuwa na akili bora kuliko nilivyodhanika alikuwa nayo. Anajua vema kuliko kufanya hivyo. Mwajua, jamaa aliyeinuka wakati mmoja mkutanoni, kulifanya, alipooza. Wakambeba wakamtoa nje.

304 Kamwe haijanilazimu kuhofia chochote, kwa sababu ninaamini Yakini yangu ni Neno la Mungu. Imedhihirishwa. Juu ya Hili nitaweka nafsi na mwili wangu. Kwa nini? Hajawahi kuniambia jambo moja ila lile lililokuwa ni la Kimaandiko kabisa. Hajawahi kuniambia jambo moja, mbele ya yeyote wenu...Nitamwapisha yeyote wenu. Hivi Yeye amewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ila lililotimia? Hiyo ni hakika.

305 Ni kitu gani? Ni, "Juu ya mwamba huu," juu ya Neno hili. Huo ndio Ule ambapo ninapata ufunuo. Ni kutoka Kwake Yeye anayeufunua. Sina elimu. Mimi sijaribu kusoma, sijaribu kulijua. Mimi hufanya tu vile Yeye anavyoniambia. Halafu, anaponionyesha, ninaangalia *hapa*, nalo Hilo hapo. Hata sikuliona, na Hili *hapa*, na Hilo linajidhihirisha Lenyewe. Hiyo ndiyo Yakini yangu. Imenidumisha kote katika miaka hii. Ndugu, imenisaidia wakati sikuwa na njia nyingine ya kusaidika.

306 Ninataka kufa Kwake. Nitakapofikia wakati wa kufa, natumaini, kama Musa, nitauona huo Mwamba umesimama kule. Ninataka kusimama juu yake, na kuwa na wabeba jeneza fulani watakaonibeba.

307 Mpaka wakati huo basi, nitaishi mkweli kwa Neno hilo, kwa hiyo nisaidie, Mungu, kwa sababu hiyo ndiyo Yakini yangu, pasipo na kijicho kwa mtu yeyote, pamoja na upendo na neema kwa wote. Kama hiyo si kweli, Mungu angeweza kuniua nikisimama hapa katika mimbara hii. Sina kijicho na mtu yeyote. Ninampenda kila mtu.

308 Basi hamjui, hivi mliwahi kusoma Yohana wa Kwanza 4:17, ya kwamba inawapasa kupata marekebisha kama hayo, kufanya pendo la kweli wakati wa hukumu? Sio ati niwe tofauti. Ni upendo. Upendo ni mkali, na upendo hurudi.

309 Mtu, ambaye angemruhusu mke wake kutoka na kukimbia huku na huku usiku kucha pamoja na walevi fulani, aingie, kesho yake asubuhi, aseme, "Ndiyo, kipenzi, natumaini ulikuwa na wakati mzuri," wewe ni mwanamume duni sana.

Mwanamume yeyote ambaye angemruhusu mke wake atoke huko nje na kuvaa kaptura, na maskini suti hizi za kuogelea, mabikini, ama chochote kile, akae miongoni mwa hawa watu, nina matumaini duni sana ya wewe hata kuwa mwanamume. Hiyo ni kweli.

³¹⁰ Mwanamume hapimwi kwa kiasi cha misuli ya mikono yake, jinsi misuli yake ilivyo mikubwa. Yeye anapimwa kwa tabia yake. Hiyo ni kweli kabisa. Nayo tabia hutokana na Neno la Mungu, na hilo peke yake.

³¹¹ Pia mhubiri yeyote anayedai kuwa ni mhubiri, akikana Neno hilo, ni tabia ndogo ya Mungu pale, kwangu mimi. Amina. Huenda kukawa na matumaini kama atasikiliza kwa muda kidogo. Naam. Sasa, sitaki kuwa mkosoaji tena. Mnaona? Ninawapenda, nami ninamaanisha hilo.

³¹² Lakini Hilo ndilo Yakini yangu, ndugu zangu, Neno hili, BWANA ASEMA HIVI. Nanyi mnajua hiyo ni kweli.

³¹³ Nilikuwa nikiangalia kila mahali nimwone Ndugu Carlson, nione kama alikuwa angali ameketi hapa. Nadhani ameondoka. [Mtu fulani anasema, "Henry?"] Naam. Alikuwa akizungumza hapa, muda mfupi uliopita.

³¹⁴ Yeye alikuwa moja kwa moja kule Chicago wakati kundi hilo la Ushirika Mkuu wa Wahudumu wa Chicago, mbona, siku mbili ama tatu, walikuwa wanivute mle ndani na kunichunguza vikali, naam, juu ya mambo fulani ambayo nilikuwa nikifundisha juu ya Hili na kuhusu mambo haya. Basi siku tatu usiku kabla halijatukia, Roho Mtakatifu aliniamsha na kusema, "Nenda pale ukasimame karibu na lile dirisha." Nikaenda, na kulikuwako na radi iliyokuwa ikimemetesha. Akasema, "Wana mtego waliokuwekea, lakini usikose kwenda. Nitakuwa pamoja nawe."

³¹⁵ Nikamchukua Ndugu Carlson, Ndugu Tommy Hicks. Nyote mnamfahamu. Tunayo kanda yake papa hapa. Nao walitaka mimi niende kesho yake asubuhi, kula kiamshakinywa pamoja nao. Nikashuka chini kwenye Mji na Nchi, nasi tukaketi chini kule. Nilidhani nitamkagua tu Tommy. Yeye ni rafiki yangu msiri, ndugu wa thamani. Nikasema, "Tommy, inanibidi kukutana na hao wahudumu." Nikasema, "Wewe ni Daktari wa Uungu. Maskini njia yangu ya kijinga ya kuzungumza," nikasema, "Nisingeweza kukutana na jamaa hao. Hivi huwezi kufanya jambo hilo kwa ajili yangu? Nimekufanyia fadhila nyingi."

Kasema, "Loo, siwezi kufanya hivyo, Ndugu Branham."

³¹⁶ Naye Ndugu Carlson, hao, wakaangaliana. Nikasema, "Mnafikiri mnanificha hilo? Ninajua ni kwa nini usingefanya hivyo." Nikasema, "Sikilizeni. Ni kwa sababu Shirika hilo lina jambo fulani ambalo wataniuliza maswali juu yake." Nao wote

wawili wakaonekana kana kwamba wangaliweza kuanguka kupitia sakafuni.

317 Basi walipofanya hivyo, nikasema, “Hakika, ndivyo. Lakini, hebu niwaambie, Ndugu Hank.”

318 Yeye ameketi hapa mahali fulani sasa. Yuko papa hapa karibu. Na kwa hiyo ameketi papa hapa. Nikasema, “Ndugu Hank...” Acheni ashuhudie. Na kwa hiyo ndiyo kwanza tumalize kulizungumzia, muda mfupi uliopita, kule ndani.

319 Nikasema, “Ndugu Hank, sikiza. Mmekikodisha kile chumba cha hoteli, sivyo? Lakini BWANA ASEMA HIVI, watawakatalia.”

Akasema, “Ndugu Branham, wamepokea amana yangu.”

320 “Sijali kile ulichopeleka huko. Hutakipata. Tunaenda mahali fulani... Palipo na chumba cha kijani, na *hiki* ni cha hudhurungi. Naye Dk. Meade ataketi hapa, na *fulani-na-fulani*,” na mahali hasa watakapokuwa wameketi. Kisha nikasema, “Sitaki wewe ujaribu kunitetea hata kidogo. Nitambulishe tu kwa kusanyiko, kisha uniache nifanye yaliyosalia.” Akasema...

321 Basi asubuhi hiyo wakati alipokuja pale, kila mtu akiwa ameketi vivyo hivyo hasa. Walipabatilisha mahali hapo. Basi ilimbidi kupata mahali pa Mji na Nchi huko nje, ku—kupapata mahali hapo, chumba cha hudhurungi, vivyo hivyo hasa. Hapo aliketi Dk. Meade na hao wengine wote, mahali tu ambapo wao...

322 Nikamwangalia, naye Ndugu Tommy Hicks akaniangalia. A—a—a—akasema, “Ndugu Branham, ninajisikia kama kuzimia.” Kisha kasema...

Nikasema, “Usiwe na wasiwasi.”

323 Hivyo basi Ndugu Carlson akasimama, kasema, “Sasa, ninajua wengi wenu ninyi watu hamtakubaliana na Ndugu Branham, na mambo kama hayo,” lakini kasema, “lipo jambo moja, yeye haogopi kusimama hapa.” Kisha kasema, “Sasa, nitampa yeye nafasi.”

324 Nikasema, “Sasa, kila mmoja wenu, haya hapa ndiyo mliyo nayo dhidi yangu.” Nami nikataja, mambo manne au matano mbalimbali. Nikasema, “Nataka mtu fulani aichukue Biblia Yake aje hapa, asimame karibu nami na kuyakanusha. Hakika. Na kama hamwezi kufanya hivyo, basi ondokeni mgongoni mwangu.” A—ha. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Naam, bwana. A—ha! Hiyo ni kweli.

325 Nilikuwa nimesimama huko Bombay, India, juu ya jambo lilo hilo, wakati kipofu mmoja alipokuwa amesimama pale. Hao mamajusi na kadhalika wameketi huko nje, nao, watu watakatifu, na Waislamu, na Wabudha, kila kitu. Tayari nilikuwa nimeona ono mtu huyu angefunguliwa macho yake. Nikasema, “Hebu, mmoja wenu ninyi watu huko nje, aje hapa

akayafungue macho yake. Nilikaribishwa leo hii na dini kumi na saba mbalimbali, na kila mmoja wenu anamkana Yesu Kristo.” Nikasema, “Kama dini yenu ni kubwa sana, njoni, yafungueni macho ya mtu huyu.”

³²⁶ Mngesema nini? Yeye alikuwa ni mwabudu jua. Kama, Roho Mtakatifu, lakini walidhani Huyo alikuwa ni “telepathia,” mnaona, nami ati nilikuwa “nikisoma nia yao.”

³²⁷ Nikasema, “Mbona, hakika Mungu wa maumbile, kama mtu anataka kufanya yaliyo haki, hakika kwamba Mungu wa maumbile atamrejsha katika hali yake nzuri.”

³²⁸ Nisingesema hivyo, bure, kama sikuwa nimeliona hilo likitukia katika ono. Lakini, nilijua, basi. Mnaona? Hutaki kuchukua kitu unachowazia. Unataka kuwa na hakika kabisa ya kwamba unasema kweli, ndipo hujali nini kinachokuja wala kinachotoka. Yeye amesimama hapo pamoja nawe, na kwa hiyo inaleta tofauti gani? Hapo, mnajua yaliyotukia, ndipo huyo kipofu akafunguliwa macho.

³²⁹ Yapata miezi miwili au mitatu iliyopita, nilikuwa nimesimama chumbani. Nikasikia sauti ikinena kwenye kona. Nikajaribu kumwamsha mke wangu, aiangalie pale. Hapo, imekuwa ikienda awali pale, palikuwa na kitu cha kuchukiza kimesimama pale kitandani, kikinishtaki. Baada ya Yeye kuniambia... Nilikuwa nimeona mamba mkubwa akikimbia. Huyo ni nyoka wa Kiafrika, naye alikuwa akijaribu kuwaua watu, naye alikuwa akimfuata ndugu yangu. Ndipo nikapiga makelele, “Ee Mungu, nifanye nini?”

³³⁰ Akasema, “Umepewa nguvu za kumfunga.” Kasema “Uwe na moyo wa ushujaa.”

³³¹ Nilizungumza naye. Ndipo mkia wake ukainuka hewani, naye akajinyonganyonga hapo, na, kama tu mkono wa gudulia hili hapa, na akajisonga roho akafa. Moshi wa samawati ukatoka kwake.

³³² Kesho yake asubuhi, nilipoamka, nilikuwa nimelala pale. Nikasema, “Afadhali niamke na kuwapeleka watoto shuleni.” Nikatazama huko, na kulikuwa na kitu hiki cha kuchukiza sana. Ilionekana kana kwamba ilikuwa ni Alley Oop kwenye lile gazeti la vichekesho, pembe kubwa mno zikitokeza kwake. Alikuwa akienda, alisikika kama kuku akilia, ama—ama kuimba, kana kwamba wanatoka kwenye banda. Nikamwangalia.

Nikasema, “Meda, Meda, mpenzi.” Naye hakuamka.

³³³ Nikawaza, “Naam, hicho kingemshtusha hata kufa.” Nikangojea pale kwa dakika moja tu, na kusimama na kuangalia.

³³⁴ Watu huzungumza kuhusu pepo, na hata hawajui hao ni nini, wakati mwingine. Hiyo ni kweli. Lakini unakabili na nao moja kwa moja, kila siku, labda, lakini utakabili na nao. Angalieni.

335 Basi baada ya kitambo kidogo, yeye alikuwa akinishtaki. Kasema, “Huna nguvu pamoja na Mungu. Wewe ni mdanganyifu tu. Huna nguvu.”

336 Nikasema, “Shetani, wewe ni chukizo kwangu. Niondokee, katika Jina la Yesu Kristo.” Naye akaondoka.

337 Nikalala pale kidogo, kitandani. Nikaanza kuamka, nikahisi hisia tamu kwelikweli ikija juu yangu. Nikawaza, “Sijui kama Roho Mtakatifu sasa yuko karibu?” Ndipo hapo pembeni... Hivyo anisaidie, hii hapa Biblia yangu juu ya moyo wangu. Sauti tamu kuliko zote niliyopata kusikia maishani mwangu, ilisema, “Usiogope kwenda popote, na usiogope kufanya lolote, kwa kuwa Uwepo wa Yesu Kristo usioshindwa uko pamoja nawe popote uendapo.”

338 Hilo lilitosha, kwangu mimi. Acha wavume. Nina Yakini. Nanga yangu inashikilia huko, kwa sababu ni Neno la Mungu aliye hai. Amina. Naam. Mnamwamini?

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

339 Ikiwa huna hiyo Yakini sasa, ipate. Kama ungetaka kuwa na hiyo Yakini, hilo hakikisho moyoni mwako la Roho Mtakatifu, inua mkono wako, useme, “Ninataka kitu ambacho kitaitikia Neno la Mungu, nami ninaweza kuona Neno la Mungu likidhihirishwa.” Amina. Mungu awabariki. Ni kote jengoni. Asanteni.

340 Ninakwambia tu Ukweli, rafiki. Usiache Hilo likupite. Sidai... Mimi si kitu. Mimi ni ndugu yenu. Msimjali mjumbe hata kidogo. Ninyi angalieni Ujumbe. Msimwangelie mjumbe. Mungu atamwondoa huyo kutoka kwenu. Yeye hatashiriki Utukufu Wake na mtu yeyote. Hiyo ni kweli. Msimwangelie mjumbe. Uangalieni Ujumbe.

341 Kama mtu akikimbia akaingia hapa, huenda akawa ni mweusi, manjano, hudhurungi, aliyeparuza, kama ana hundi kwa ajili yako kwa hati ya benki ya dola milioni moja, usingejali alikuwa ni wa rangi gani ama jinsi alivyovalia. Ni ule ujumbe alio nao kwa ajili yako.

342 Sasa, msiangalie sarufi yangu na—na kadhalika. Ninyi kumbukeni tu ninawaambia kuhusu Yesu Kristo Yule aliyepo hapa sasa. Mwaminini kwa moyo wenu wote. Msikose kumwamini.

343 Ninaangalia sasa nione kile atakachoniambia. Endeleeni tu kuinamisha vichwa vyenu na muanze kuomba. Iweni tu na imani. Msitie shaka.

344 Sasa, Baba wa Mbinguni, yote yako mikononi Mwako. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, sasa hivi tu, ya kwamba wanaume na wanawake hapa ndani waweze kutambua ya kwamba hili si jambo rahisi kufanya, ukiwa mwanadamu na ukiishi miongoni mwa wanadamu, ukiishi pamoja na watu.

Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba wataelewa hili na kujua ya kwamba mtumishi Wako a—anajaribu kuzungumza habari Zako. Nami nimeona ya kwamba Wewe hulitimiza Neno Lako, Bwana. Nimeona kwamba ni kweli. Nimeona kwamba Wewe na Neno Lako ni mmoja.

³⁴⁵ Nawe umenileta salama umbali huu, Baba. Kama... Yule Malaika Ambaye watu wamemwona, na kuiona Nuru Yake, Yuko katika Nguzo ya Moto. Bwana, kwa moyo wangu wote ninaamini ni Bwana wetu Yesu Kristo. Ninaamini Huyu ni Roho Wake, Roho Mtakatifu, ambaye sote tunamwabudu na kumwamini.

³⁴⁶ Mungu, jalia tusikose kumtambua sasa, pia jalia tufahamu na kurudi. Na jalia kanisa lijisafishe. Jalia kila dhehebu. Baba, siombi ya kwamba Wewe utayavunjilia mbali madhehebu hayo. Bali ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu ataingia kwenye madhehebu hayo, nayo yatakuwa yanaona mambo kitofauti, ili wote wapate kuwa mmoja, udugu. Tujalie.

³⁴⁷ Ninakushukuru kwa ajili ya ushirikiano wao mzuri, Bwana. Kama isingalikuwa ni Wewe katika jambo hili, hakuna mtu angalini karibisha. Lakini, Wewe, Wewe ulinipa kibali na wahudumu hawa. Naomba ya kwamba utawabariki, Bwana. Ninawaombea, zaidi sana, kwa ajili ya kila mmoja.

³⁴⁸ Ninamwomba Ndugu Williams. Bwana, mpe shauku ya moyo wake. Loo, ninaomba ya kwamba Wewe utamsaidia, yeye na Dada Williams, na—na shauku zao. Ndugu Shakarian, Dada Shakarian, viongozi hawa wote hapa, wa kundi hili lote kubwa la walei ambao umewaita watoke, katika siku hizi za mwisho, kuubeba ujumbe wa kuwaunganisha ndugu pamoja, Bwana, jalia kamwe wasifanyike dhehebu. Jalia wakae huru na mambo haya yote, na kunyosha mikono yao na kuwaingiza ndugu wote waliozaliwa kwa Roho. Tujalie.

³⁴⁹ Yabariki makundi yote. Wabariki wa Umoja, na ninii—na ninii... makundi yote madogo mbalimbali, Bwana, yaliyo na mawazo yao mbalimbali, wa—wa Utatu, na wale wanaoamini kwamba Mungu ni wawili, na Mungu ni watatu. Na Mungu ni... Loo, lolote wanaloamini, Mungu, jalia wajue ya kwamba kuna Mungu mmoja wa kweli, Yesu Kristo ndiye Mwana Wake. Pia jalia, Bwana, ya kwamba wataweza kuyafahamu mambo haya, ya kwamba hatuna Mungu wanne ama watano. Tunaye Mungu mmoja katika—katika ofisi tatu; Mungu yeye yule, katika Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Jalia wao... Jalia huo ufunuo uwapambazukie leo, Bwana.

³⁵⁰ Jalia ugomvi huu uache kuendelea. Pia jalia wanaume na wanawake waweze kushirikiana pamoja, na wawe mmoja katika Kristo, kwa maana muda umeenda sana kwa ubishi huu na mambo madogo.

³⁵¹ Ninakuamini Wewe. Pia ninaamini, Baba, wote uliowakusudia tangu zamani wapate Uzima wataisikia Sauti

Yako na kuja. “Kondoo Wangu wataisikia Sauti Yangu.” Nami ninaamini ya kwamba utalijalia, Bwana. Wabariki sasa.

³⁵² Kunayo mikono mingi hapa ndani, ambapo labda mikono mia mbili imeinuliwa juu hewani, ambao walitaka kukupokea kama Mwokozi wao, na walitaka kukupokea Wewe kama—kama ninii yao—ninii yao—Yakini yao, kitu ambacho wangeweza kuweka imani yao juu yake, ambacho moyo wao wenyewe ungeitikia kila Neno na kulidhihirisha. Tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba.

³⁵³ Sasa, wakati mkiwa hapa pamoja na katika kundi hili dogo, ninawatakeni mwe mkiomba. Na sijawahi kufanya hili, lakini najisikia kuongozwa kulifanya. Endeleeni tu kuomba.

³⁵⁴ Basi ni wangapi wenu ninyi watu hapa ndani mnaonifahamu mimi? Nawe ni mgonjwa ama una haja, kwa ajili yako mwenyewe ama mtu fulani, inueni mikono yenu. Kwamba unanijua mimi, na unajua kwamba ninakujua, inueni mikono yenu, kila mahali. Mnaona? Inaonekana tu kama ni kote huku. Sasa, wekeni mikono yenu chini.

³⁵⁵ Sasa, wale mnaojua ya kwamba hamnijui, nami siwajui, inueni mikono yenu. Loo, bado, kila mahali, hamna njia ya kuwatofautisha.

³⁵⁶ Sasa ninawatakeni muombe, ombeni kwa uaminifu. Msitie shaka sasa. Ombeni tu. Na hebu tumwache Roho Mtakatifu. . .

³⁵⁷ Sasa, kama nimesema mambo haya, sasa, mnajua vizuri na vema haiwezekani kabisa kwangu mimi kujua wewe ni nani, kile ulicho, ama chochote kulihusu, shida yako ni nini. Lakini kunafanyika nini? Hivi Yesu hakuahidi jambo lili hili katika siku ya mwisho? Hivi Yeye hakusema pale, wakati aliposema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodom?”

³⁵⁸ Wakati Mungu alidhihirishwa katika mwili, Mtu yule aliyekuja kule, Mtu tu, akila nyama ya ng’ombe ama ndama, akinywa maziwa, na mkate. Na Yeye akasema, “Yu wapi Sara?”

Akasema, “Yuko hemani, nyuma Yako.”

³⁵⁹ Naye akasema yale alikuwa anaenda kufanya. Akasema, “Nitakutembelea.” Ibrahimu alimwita *Elohimu*, Bwana Mungu. Na Yeye akasema. . .

Sara akachekeka kifichifichi.

³⁶⁰ Ndipo Yeye akasema, “Kwa nini Sara akachekeka?” Huku mgongo wake umeelekezwa kwenye hema.

Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa. . .”

³⁶¹ Mnaona, kulikuwako na kanisa la kawaida, kanisa la kawaida, ambalo lilikuwa ni Lutu na kundi lake. Walikuwa na Billy Graham mamboleo aliyeshuka huko chini, na—na kadhalika, na Oral Roberts na hao wengine, wakiwaita watoke.

Walifanya mwujiza, kiasi kwamba, wapate kuwapofusha. Walihubiri Injili.

³⁶² Pia kulikuwako na Wasodoma. Daima kuna makundi matatu ya watu. Wasodoma, mnaona waliyofanya.

³⁶³ Lakini wateule, wapentekoste, wanavyojiita, hao walikuwa ni Ibrahimu, ambao tayari wako nje ya Misri, wametoka Sodoma tayari, wameketi katika nchi, kwenye nchi isiyo na rutuba. Mnaona aina ya Ujumbe waliopata?

³⁶⁴ Sasa angalieni, leo hii, ni lini kuliwahi kuwa na wakati? Niambieni ambapo wakati ulipata kutoka Sodoma.

³⁶⁵ Kumbukeni, huyo alikuwa ni Ibrahimu, A-b-e-r-h-a-m, ama A-b-r-a-h-a-m, hasa.

³⁶⁶ Ni wakati gani kuliwahi kuwa na mjumbe aliyeenda kwenye makanisa ya kimadhehebu ya mashinani pamoja na mtu ambaye jina lake liliishia na h-a-m, G-r-a-h-a-m?

³⁶⁷ Vipi kuhusu kwa kundi la kipentekoste? Halijawahi kujulikana katika historia. Nililipitia hilo hivi majuzi tu, nikiyachunguza majina.

Mnasema, “Majina hayamaanishi chochote.”

³⁶⁸ Kwa nini Sauli basi jina lake likabadilishwa likawa Paulo? Kwa nini Simoni kuwa Petro? Kwa nini Yakobo likawa Israeli? Hakika, lina maana.

³⁶⁹ Mwaminini Mungu. Msipuuze kitu ambacho Mungu anajaribu kuwapa. Sasa ombeni. Semeni, “Bwana Yesu, uturehemu.”

³⁷⁰ Kama sijakosea, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, ninaangalia hapa. Nafikiri yule ni Dada Carl Williams aliyeketi hapa mkono wangu wa kuume. Hiyo ni kweli, Bibi Williams? Mimi... Huku, Dada Carl Williams? Ilionekana kama ni yeye aliyeketi kule mkono wangu wa kuume. Sikuwa na hakika. Nililifanya dhahiri? Nadhani halikuwa.

Ninajaribu kumwona mtu ninayemjua.

³⁷¹ Nikiangalia kote, namwona Ndugu na Dada Dauch wameketi hapa, bali wametoka kanisani.

³⁷² Huyo ni Bibi Outlaw hapa mkono wangu wa kushoto? Huyo ndiye nilifikiri nyinyi nyote mlikuwa, anayesimama pale. Bibi Outlaw, ninakujua. Wewe ni mtu nimjuaye. Ninataka kukuuliza jambo fulani. Niangalie mimi moja kwa moja. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Unaamini ya kwamba mambo haya ninayofundisha ni Kweli? Sasa, Bibi Outlaw, sijapata kuzungumza nawe kadiri nijuavyo mimi, kwa zaidi ya mwaka mmoja, tangu nilipokuwa hapa hapo kabla. La, ninaamini nilikupungia mkono, hivi majuzi, mkahawani.

³⁷³ Angalia hapa kwangu. Lakini una mzigo moyoni mwako, si sana kwa ajili yako, bali ni kwa ajili ya mtu mwingine. Huyo

ni msichana. Ni binti mkwe wako. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia shida ya huyo binti mkwe? Ana namna fulani ya ugonjwa wa mapindi, na pia ana wasiwasi, wasiwasi sana, sana. Vema. Usi—usiwe na wasiwasi. Utamwacha. Alihisi hilo papo hapo, akiketi hapa. Naam. Utamwacha.

³⁷⁴ Kuwa tu na imani. Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”]

³⁷⁵ Huyu hapa mama ameketi moja kwa moja chini mbele yangu hapa, mgeni kabisa. Lakini hivi hamwezi kuiona hiyo Nuru inayoning’inia juu yake? Anaugua udhaifu mwilini mwake. Yeye, hatoki hapa. Anatoka California. Mimi ni mgeni kabisa kwa mwanamke huyo, lakini anajua ninazungumza naye sasa. Mnaona hiyo Nuru inayoning’inia juu yake? Mimi... Simjui, sijawahi kumwona. Lakini jina lake ni Bibi Elliott. Kama utaamini kwa moyo wako wote, nenda nyumbani, upate afya. Unaamini? Vema. Sasa, kama mimi ni mgeni na kila kitu, pungu mkono wako, pia, namna *hiyo*. Mnaona? Inua mkono wako, na uamini kwa moyo wako wote, uone kama hiyo ni sawa. Kuwa na imani.

³⁷⁶ Huyu hapa mama ameketi papa hapa mbele yake, papo hapo karibu naye, hapana shaka ni mumewe. Ameketi hapo pia, naye ana shida ya misuli yake. Ina mishtuko ya ghafla ndani yake. Hiyo ni kweli. Naam, mama. Bibi Darwich, kama ukiamini kwa moyo wako wote! Unaamini? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Haya basi. Sikujui, sijawahi kulijua jina lako wala chochote kulihusu, bali hiyo ni kweli. Sivyo? Nawe ulikuwa umeketi hapo, ukisema, “Bwana, na iwe ni mimi.” Mnaona? Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako huku na huku, namna *hii*. Punga mkono wako kama hiyo ni kweli. Vema.

³⁷⁷ Haya basi. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Baba wa Mbinguni anajua mambo hayo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ni kitu gani? Ni Yesu Kristo. Linafanya nini? Hivyo ndivyo hasa Yeye alisema lingefanya katika siku za mwisho.

³⁷⁸ Sasa, kama hiyo ni kweli, na Mungu analitenda, akionyesha kwamba ni kweli, basi Neno ninalohubiri ni kweli, kwa sababu ni Mungu yeye yule akilitimiza Neno Lake. Mwaminini Bwana.

³⁷⁹ Geukeni kutoka kwenye njia zenu vuguvugu. Yaondokeeni mambo haya yanayowakokota nje, kama Hollywood, mambo hayo yanayowakokota kama makanisa hayo mengine. Mrudieni Mungu, na mpate yakini itakayoshikilia nanga ya moyo wenu.

³⁸⁰ Ni wangapi wangependa kuwa na tukio hilo pamoja na Kristo? Simama kwa miguu yako papa hapa katika Uwepo Wake, ambapo unajua Yeye yupo hapa. Mungu awabariki. Mungu awabariki. Sasa, hilo ni sawa. Sasa, hilo ni zuri sana. Loo, jamani! Sijui la kusema.

³⁸¹ Kama kila mmoja wenu hapa atakubali Ujumbe huo, ya kwamba Yesu Kristo yupo papa hapa pamoja nasi! “Bado

kitambo kidogo na ulimwengu, wasioamini, hawataniona tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona. Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Hiyo ni kweli? Vema, mnamwona akifanya kazi, yale hasa aliyoahidi.

³⁸² Sasa, Yeye yupo hapa. Jambo pekee linalokupasa kufanya, ni usininii tu. . . Jilaze tu chini na kusema, “Bwana Yesu, sasa ninakusudia moyoni mwangu, tangu saa hii na kuendelea, mimi ni Wako, na Wewe ni wangu. Nami ninataka tukio hili moyoni mwangu, kusudi niweze kunena Neno Lako, Neno Lako litaishi. Na yale ninayoomba, ninaamini yatatimizwa.” Mnautaka?

³⁸³ Basi hebu tuinue tu mikono yetu kwa Mungu na kuomba, kila mmoja wetu sasa, kila mtu. Halafu ninawatakeni muinue mkono mmoja juu, na kuweka mkono mmoja juu ya mwingine karibu nawe. Sawa. Hilo ni sawa.

Wafanyabiashara, Mungu daima awabariki, awe pamoja nanyi!



63-0127 Yakini
Ramada Inn
Phoenix, AZ Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org